# IKULU ZANZIBAR

SERIKALI KWA MAENDELEO YA WANANCHI

TOLEO NO. 021 ISSN 1821 - 8253 MEI - JUNI 2015



# Dk. Shein alivunja Baraza la 8 la Wawakilishi

## Bodi ya Wahariri

**Mhariri Mkuu**
Hassan K. Hassan

**Mhariri Msaidizi**
Ali S. Hafidh

**Waandishi**
Said J.Ameir
Rajab Y. Mkasaba
Haji M. Ussi
Said K. Salim
Yunus S. Hassan
Mahfoudha M. Ali
Amina M. Ameir

**Mpiga Picha**
Ramadhan O. Abdalla

**Msanifu**
Aziz I. Suwed


## UTAMBULISHO

Wapenzi wasomaji wa Jarida la Ikulu tunafuraha kukukaribisheni katika uendelezaji wa juhudi za Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuimarisha mawasiliano na wananchi.

Ni lengo la Ofisi ya Rais kukuza mawasiliano na wananchi kwa kutumia njia tofauti kama vile Jarida, vipeperushi pamoja na vyombo vyengine vya habari.

Tunakaribisha maoni yenu ili tuweze kufikia lengo hilo.


Jarida hili limetolewa na Idara ya Mawasiliano Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar.

P.O.BOX: 2422

Zanzibar - Tanzania

Phone: +255 223 081/5

Fax: 024 223 3722

Email: com_ikulu@ikuluzanzibar.go.tz


# Maoni ya Mhariri

## Tuzisimamieni sheria zetu zinazotuongoza

Zanzibar kama zilivyo nchi nyengine nyingi za Bara la Afrika, imejiwekea misingi mizuri ya sheria katika kuendeleza masuala yake mbali mbali yakiwemo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Sheria nyingi miongoni mwa sheria zinazotumika kuongoza sekta hizo ama zimerithiwa na kutumika kama zilivyo kutoka kwa watawala wa kikoloni miaka iliyopita, au zimefanyiwa marekebisho ili kuweza kukidhi mahitaji na mazingira ya wakati uliopo kwenye nchi husika. Sheria hizo zimekuwa zikiendelea kutumika na kuleta ufanisi mkubwa katika suala zima la utawala wa sheria kwenye baadhi ya nchi.

Wataalamu wa masuala ya sheria wamethibitisha kuwa hakuna sheria ambayo kwa ukamilifu wake itakuwa mpya bila ya kufuata misingi ya sheria zilizokuwepo kabla, jambo ambalo linajidhihirisha kwenye sheria hizo ambazo nyingi zao huweko kwenye lugha za kigeni.

Kimsingi, hakuna taasisi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo imekuwa ikiendeshwa bila ya kuwa na sheria inayoiongoza taasisi hiyo. Inawezekana kwamba baadhi ya sheria zinazotumika zimepitwa na wakati na ndipo inapokuja haja ya kuzifanyia mapitio baadhi ya sheria ili ziweze kurekebishwa. Kwa kulitambua hilo SMZ imeanzisha tume maalum ya mabadiliko ya sheria.

Aidha, kutokana na umuhimu wa kuimarisha utawala wa sheria unaoheshimu haki za binadamu pamoja na utumishi wa umma uliotukuka, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukua hatua kadhaa muhimu za kuimarisha sheria za nchi.

Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na kupitisha Sheria ya Nam. 2 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011, Sheria Nambari 2 ya mwaka 2012 ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, Kukamilika kwa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kufuatia mswada wa Sheria hiyo uliopitishwa na Baraza la Wawakilishi, tarehe 30 Januari, 2015 na sheria nyingine nyingi.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, katika kutekeleza wajibu wake wa kuhakikisha kuwa kunakuweko na utoaji wa haki katika vyombo vya sheria, imechukua hatua maalum za kuiimarisha Mahkama.

Kwa upande wa majaji, Serikali imefanikiwa kuongeza idadi yao kutoka wawili mwaka 2011 hadi sita mwaka 2014, sawa na ongezeko la asilimia 200. Vile vile Serikali imefanikwa kuongeza idadi ya Mahakimu wa ngazi mbali mbali kutoka 43 mwaka 2010 hadi 85 mwaka 2015. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 97.7. Kadhalika, Serikali imeiongeza bajeti ya Mahakama kutoka TZS bilioni 1.3 mwaka 2010/2011 hadi TZS bilioni 5 mwaka 2013/2014. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 284.6.

Ni dhahiri kuwa, juhudi hizi za Serikali, ni kielelezo thabiti cha kuhakikisha kuwa mahakama zinaendelea kuwa huru, zinafuata misingi ya utawala bora na zinakwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia, kiuchumi na kijamii yanayoendelea kutokea ndani na nje ya nchi.


Lakini je, ni kwa kiasi gani jihudi hizi za kuimarisha misingi ya sheria zimesaidia kuongeza ufanisi, utawala wa sheria na kuharakisha maendeleo?

Pamoja na juhudi zinazochukuliwa na Serikali, bado zipo changamoto kadhaa zinazohitaji kupatiwa ufumbuzi ili Serikali iweze kufikia malengo iliyokusudia. Bado kuna udhaifu mkubwa katika kuzisimamia sheria hizo jambo ambalo limekuwa likisababisha malalamiko mengi kutoka kwa wananchi mbali mbali ambayo msingi wake yanatokana na kutosimamiwa ipasavyo misingi ya sheria ambazo tumezianzisha wenyewe.

Akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kuwasili nchini kutoka ziara yake ya kikazi nchini Ujerumani, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein amesema matatizo mengi ya Zanzibar yanasababishwa na watu kushindwa kuzitii na kuzisimamia sheria za nchi kutokana na muhali na kujuana.

Alisema kwa mfano sheria za usafi ambazo zinaongoza Manispaa za miji ya Zanzibar ndizo hizo hizo zinazotumika katika miji mingine duniani, lakini hali halisi ya usafi kwenye miji ya Zanzibar inaonekana tofauti na miji mingine kutokana na watu kupuuza sheria na wale wanaozivunja kushindwa kuchukuliwa hatua za kisheria.

Hivyo ufumbuzi wa matatizo mengi ya Zanzibar unaweza kupatikana kwa kuzitii na kuzisimamia ipasavyo sheria zilizopo bila ya kuoneana muhali kwa kujuana.



# Dk. Shein alivunja Baraza la 8 la Wawakilishi



# Abainisha mafanikio ya utekelezaji wa Ilani ya CCM 2010 – 2015

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein amefafanua mafanikio ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba, katika nyanja zote za maendeleo, kisiasa, kiuchumi na ustawi wa jamii, ambao unahusisha utekelezaji wa Ilani ya CCM 2010 – 2015 pamoja na ahadi mbali mbali alizozitoa wakati alipokuwa akilivunja Baraza la Nane la wawakilishi mwezi Novemba 2010.

Katika hotuba yake aliyoisoma wakati wa kulifunga Baraza hilo, Dk. Shein amesema siri kubwa ya mafanikio hayo yanatokana na mchango wa Wajumbe wa Baraza hilo katika kutekeleza wajibu wao kufuatana na Mipango mikuu ya kitaifa ikiwemo Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 – 2015 ambayo ndiyo mkataba muhimu baina ya Serikali na wananchi. Ilani hiyo imeshatekelezwa kwa kiwango kinachokadiriwa kufikia asilimia 90.

Ifuatayo ni sehemu ya hotuba ta Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati alipokuwa akilivunja Baraza la nane la Wawakilishi, tarehe 26 Juni, 2015.

**HALI YA UCHUMI:**

Katika kipindi hiki kuanzia mwaka 2010 – 2014, Pato la Taifa kwa bei za miaka hiyo limekua kutoka TZS bilioni 1,050.8 hadi kufikia TZS bilioni 2,133.5. Kwa bei za kudumu, Pato la Taifa limekua kutoka TZS bilioni 848.2 hadi kufikia TZS bilioni 1,115.4 sawa na ukuaji wa asilimia 31.5 kwa kipindi hicho. Uchumi wa Zanzibar umekua kutoka asilimia 4.3 mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 7.0 mwaka 2014 sawa na ongezeko la asilimia 2.7. Pato la Taifa kwa mwananchi mmoja, kwa bei za miaka 2010 – 2014, limekua kutoka TZS 856,000 ($613) mwaka 2010 hadi kufikia TZS 1,552,000 ($939) kwa mwaka 2014.

Katika kipindi cha mwaka 2010/2011 hadi 2014/2015, mapato ya ndani yameongezeka kutoka TZS



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akisisitiza jambo katika hotuba yake ya kuvunja Baraza la nane la Wawakilishi la Zanzibar huko Chukwani Wilaya ya Magharibi Unguja, tarehe 26 Juni, 2015*

bilioni 181.4 hadi kufikia TZS bilioni 360.4, sawa na ukuaji wa asilimia 98.7 kwa kipindi hicho au wastani wa asilimia 19.7 kwa kila mwaka. Mfumko wa bei unaendelea kuweko katika tarakimu moja. Katika mwaka 2010, mfumko wa bei ulikuwa wa wastani wa asilimia 6.1 na umeshuka kufikia wastani wa asilimia 5.6 kwa mwaka 2014.

Katika kipindi cha miaka mitano, Serikali imefanya jitihada kubwa za kuiimarisha na kuishirikisha Sekta binafsi katika mipango ya maendeleo. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tayari imeanzisha kitengo cha "PPP" katika Tume ya Mipango kwa ajili ya kushughulikia miradi itakayoanzishwa kwa mfumo huo. Serikali imejiandaa kuanzisha Idara kamili ya "PPP" ambayo itahusika na utekelezaji na usimamizi wa shughuli zote za miradi ya mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

**UWEKEZAJI VITEGA UCHUMI:**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba, kupitia Mamlaka ya Vitega Uchumi (ZIPA) ilifanya kazi nzuri katika kuwavutia wawekezaji wa nje na ndani kuja kuwekeza katika sekta mbali mbali za kiuchumi na kijamii. Kwa Kipindi cha miaka mitano (2010 – 2015), SMZ imeweza kusajili miradi 187 yenye thamani ya TZS milioni 38,560.50, sawa na USD 1,881,00 milioni ambayo inakadiriwa kuwapatia ajira watu 9,192. Wawekezaji kutoka Uturuki, China, Italia, Ujerumani na India wameonesha dhamira ya dhati ya kuiunga mkono Serikali. Mafanikio hayo yanatokana na ziara za Rais wa Zanzibar alizozifanya kwenye nchi hizo na kuwakaribisha kuja kuwekeza. Sambamba na juhudi hizo, wawekezaji wa ndani nao wamehamasika katika uwekezaji kwenye nyanja mbali mbali.

Serikali kupitia Mamlaka ya Uwekezaji na Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA), kuanzia mwaka wa fedha 2014/2015, imeweka mkazo mkubwa katika kukamilisha dhamira ya kuendeleza maeneo huru ya uchumi, mpango ambao ulibuniwa na hatimae kutolewa tangazo la Sheria Namba 5 la mwaka 1993 lakini bado hazijachukuliwa juhudi za kutosha za kutekeleza kwa vitendo mpango huo.

Mipango ya serikali ya hivi sasa ni kuibadilisha taswira ya eneo la Fumba kwa kuutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Mji wa Kisasa wa Fumba (Fumba Bay Satellite City Project). Mji huu mpya wa kisasa na wa kibiashara utakuwa na mtaa mkubwa wa biashara (High Street), nyumba za kisasa za kibiashara za kuishi wageni na wenyeji, uwanja wa kuchezea mchezo wa gofu, hoteli kubwa ya kitalii na shughuli mbali mbali za kibiashara.

Katika Mkoa wa Kaskazini Unguja, SMZ imeshaanzisha Mradi wa Maendeleo ya Mji wa Kisasa Kijini – Matemwe. Mradi huu unaendelea kutekelezwa na Kampuni ya "Penny Royal" katika maeneo ya Matemwe Muyuni, ambapo utagharimu jumla ya Dola za Kimarekani milioni 220. Mradi huo unajumuisha ujenzi wa Hoteli ya kimataifa yenye hadhi ya nyota tano. Aidha, mradi huo utahusisha ujenzi wa kiwanja cha kimataifa cha gofu, chenye jumla ya vishimo 18 na ujenzi wa nyumba za makaazi kwa watu wenye kipato cha juu ambazo zitatumia nishati ya nguvu ya upepo. Hivi sasa Kampuni hiyo inaisaidia Serikali katika ujenzi wa



*Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar wakimsikiliza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein wakati alipozungumza nao katika uvunjaji rasmi wa baraza hilo la nane Chukwani Wilaya ya Magharibi Unguja, tarehe 26 Juni, 2015*

barabara yenye urefu wa km 20.2 kutoka Matemwe kupitia Kijini kuelekea maeneo ya mradi hadi Kidoti. Ujenzi wa barabara hio unaendelea vizuri.

Katika eneo la Mjini Unguja, katika kipindi hiki, Serikali imepanga kutekeleza Mradi wa Kuendeleza Hoteli ya Bwawani na eneo linaloambatana nalo. Serikali italiendeleza eneo hilo kupitia Muwekezaji wa Kampuni ya "Quality Group" aliyeshinda zabuni. Kampuni hii inakusudia kuendeleza eneo la Bwawani kwa kujenga Hoteli ya Kisasa ya nyota tano, majengo ya kisasa ya makaazi, majengo ya biashara, mikahawa, soko la Kizanzibari na maegesho ya magari. Jengo la sasa la hoteli ya Bwawani litakarabatiwa kwa ajili ya kupokea wageni mashuhuri. Uendelezaji wa eneo la Bwawani utazingatia ipasavyo athari za Kimazingira na urithi wa kale.

**SEKTA YA BIASHARA NA VIWANDA:**

Katika mwaka 2014 Serikali imeweza kuuza nje bidhaa zenye thamani ya TZS milioni 133,591.7 kutoka bidhaa zenye thamani ya TZS milioni 87,799.6 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 52.14. Usafirishaji huo umeongezeka kwa kiasi kikubwa kutokana na jitihada za Serikali za kuimarisha uzalishaji wa zao la karafuu na mwani, ambayo usafirishaji wake ulifikia TZS milioni 103,079.2 kutoka TZS milioni 75,392.6 mwaka 2013. Hili ni ongezeko la asilimia 77.8 ya usafirishaji wote kwa mwaka 2014. Licha ya kuwepo kwa urari kwa bidhaa kwa usafirishaji nje, takwimu hizi zinatoa matumaini mazuri juu ya mwenendo na ukuaji wa biashara nchini.

Kuhusu biashara baina Zanzibar na Tanzania Bara, jumla ya bidhaa zenye thamani ya TZS milioni 23,268.7 ziliingizwa Zanzibar kutoka Tanzania Bara mwaka 2010 ikilinganisha na bidhaa zenye thamani ya TZS milioni 64,296.4 mwaka 2014. Vile vile, bidhaa zenye thamani ya TZS milioni 2,203.8 zilisafirishwa kwenda Tanzania Bara mwaka 2010 ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya TZS 366,354.2 mwaka 2014. Kwa jumla, katika kipindi hiki cha kwanza cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba, urari wa biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara unaendelea kuwa mzuri kwa upande wa Zanzibar. Ni dhahiri kuwa juhudi zilizochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba, za kufufua zao la Karafuu zimezaa matunda mazuri.

Rais wa Zanzibar ameitimiza ahadi aliyoitoa mwaka 2011 ya kuwalipa wakulima wa zao la Karafuu asilimia 80 ya bei ya karafuu ya Soko la Dunia. Karafuu za Daraja la Kwanza zinanunuliwa kwa bei ya TZS 14,000 kwa kilo badala ya TZS 5,000 kwa kilo, bei iliyokuwepo mwaka 2010. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 180. Kadhalika, vituo vipya vya ununuzi na uuzaji wa karafuu vimejengwa Unguja na Pemba, vituo vya zamani vimekarabatiwa na huduma zote muhimu zinapatikana kwenye vituo hivyo. Aidha, Serikali imefanikiwa sana katika kupambana na Magendo ya Karafuu na wananchi wanauza Karafuu zao katika Vituo vya ZSTC.

Thamani ya bidhaa zilizozalishwa viwandani imeongezeka kutoka TZS bilioni 128 mwaka 2013 hadi kufikia TZS 136 bilioni mwaka 2014. Hili



*Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ambao ni Mawaziri wa Wizara mbali mbali akiwepo Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Said Hassan Said wakifuatilia hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein wakati alipolivunja rasmi Baraza hilo la nane katika ukumbi wa Baraza hilo Chukwani Wilaya ya Magharibi Unguja, tarehe 26 Juni, 2015*

ni sawa na ongezeko la asilimia 5.5. Wawekezaji wamekuwa wakiwekeza katika viwanda vya usafishaji nafaka, usindikaji maziwa, uzalishaji sukari, maji ya kunywa na vinywaji mbali mbali. Aidha, pamekuweko na ongezeko la ukuaji wa viwanda vidogo vidogo vinavyozalishwa na wajasiriamali wanaozalisha sabuni, vifaa vya ujenzi, samani na bidhaa za viungo Unguja na Pemba.

Ukuaji huo vile vile umepelekea kuwepo kwa ongezeko la mchango wa sekta hii kwa Pato la Taifa ambapo katika mwaka 2014 ulifikia asilimia 9.9 kutoka asilimia 6.9 mwaka 2013. Taasisi ya Viwango iliyoanzishwa baada ya kupitishwa Sheria ya Viwango Namba 1 ya mwaka 2011 imeanza kazi zake katika kuimarisha bidhaa zinazozalishwa na kuingizwa nchini.

**UTALII:**

Katika kipindi cha miaka mitano, SMZ imefanikiwa sana kuiendeleza sekta ya utalii. Kwa mafanikio makubwa imeweza kutekeleza dhana ya utalii kwa wote iliyotangazwa rasmi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein tarehe 16 Oktoba, 2011. Serikali imeifanyia marekebisho Sheria ya utalii ya mwaka 2009, na kupelekea kuundwa kwa Sheria mpya Namba 7 ya mwaka 2012 ambayo inakidhi haja na kwenda sambamba na dhana ya utalii kwa wote na kutoa miongozo imara ya kuiendesha sekta hiyo.

Takwimu zinaonesha kuwa Idadi ya watalii 132,836 walitembelea Zanzibar katika mwaka 2010; ambapo katika mwaka 2014 watalii wapatao 311,801 waliwasili Zanzibar. Hili ni ongezeko la asilimia 134 katika kipindi cha miaka minne. Katika kuhakikisha usalama wa wananchi na wageni wanaotutembelea, Serikali imeandaa Mradi wa usalama katika maeneo ya Mji wa Unguja. Jumla ya fedha kwa mradi wote kwa kipindi cha miaka mitano ni Dola za Marekani Milioni 28.9. Fedha zilizotengwa kwa matumizi ya mwaka wa kwanza ni TZS bilioni 10.

**MIFUGO NA UVUVI:**

Katika sekta ya mifugo, Serikali iliweka malengo ya kuleta mapinduzi ya ufugaji ili kuongeza tija na ubora wa mazao yanayotokana na shughuli hiyo. Dhamira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwa na ufugaji wa kisasa wa ng'ombe wa maziwa, mbuzi na kuku kwa lengo la kuongeza tija na kipato cha wafugaji. Soko la maziwa sasa limekua kutokana na muwekezaji Mzalendo kufungua kiwanda cha maziwa Fumba.

Serikali vile vile, imeimarisha maabara ya mifugo Maruhubi kwa kuifanyia matengenezo makubwa, kuweka vifaa vya kisasa vya kuhifadhia mbegu bora za ng'ombe na kuendeleza mradi wa upandishaji ng'ombe kwa shindano ili kupata ng'ombe bora.

Mwaka 2010 Serikali iliahidi kufanya jitihada za kuziimarisha shughuli za uvuvi kwa kutambua umuhimu wake katika kutoa ajira, kutupatia lishe bora na kuongeza mchango wake katika Pato la Taifa. Serikali imepata mafanikio makubwa katika utekelezaji wa azma hiyo ambapo mchango wa sekta hiyo katika Pato la Taifa umefikia asilimia 7.2. Jumla ya tani 148,535 za samaki zenye thamani ya TZS bilioni 527.5 zimevuliwa hadi mwaka 2014.

Ni jambo la kutia moyo, kuona kuwa jitihada za Serikali za kushirikiana na wananchi katika kukabiliana na

vitendo vya uvuvi haramu na kuimarisha hifadhi ya mazingira ya bahari zimesaidia sana kuongeza kiwango cha samaki wanaovuliwa. Jumla ya wavuvi wapatao 2,520 wamepatiwa mafunzo ya uvuvi bora yakiwemo ufugaji wa samaki na viumbe wengine wa baharini ndani na nje ya nchi.

Wakati huo huo, zao la mwani ni miongoni mwa mazao ya baharini yenye kuipatia Serikali fedha za kigeni. Jumla ya tani 51,687 za mwani mkavu zenye thamani ya TZS bilioni 187 zimesafirishwa nje ya nchi katika kipindi hiki.

Serikali imewapatia vihori wakulima wa mwani wa Unguja na Pemba kwa ajili ya kubebea mwani. Tunafanya juhudi kuwapa nguvu wakulima wa mwani ili kuhakikisha zao hili linasarifiwa hapa nchini kwa lengo la kukuza uchumi wetu na kuongeza kipato cha wakulima wetu. Aidha, kufuatia safari yangu ya China na Vietnam niliwashajihisha wawekezaji kushiriki katika sekta hiyo. Matumaini yetu ya utekelezaji ni mazuri.

**KAZI, AJIRA NA UTUMISHI WA UMMA:**

Katika kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana na wanawake na kuwajengea uwezo wa kipato wananchi, katika kipindi hiki cha miaka mitano Serikali imeanzisha Mfuko wa Uwezeshaji hapo tarehe 21 Disemba, 2013 ukiwa na jumla ya fedha TZS bilioni 2.413, baada ya kuunganishwa Mfuko wa Kujitegemea, Mfuko wa JK na AK na Mfuko wa Vijana. Kati ya fedha hizo, TZS milioni 973 zilipatikana kwa kuchangishwa kupitia Kamati iliyoundwa na Mheshimiwa Rais, TZS bilioni 1.2 zilitokana na mfuko wa AK/JK na jumla ya TZS milioni 140 ni fedha za Mfuko wa Rais wa Kujitegemea na TZS milioni 100 zilitokana na Mfuko wa Vijana. Lengo kuu kuunda Mfuko wa Kujitegemea ni kuwa na Mfuko ulio imara zaidi katika kuwasaidia vijana, wanawake na vikundi mbali mbali vya wajasiriamali katika shughuli zao za kujiendeleza kiuchumi.

Vile vile katika kipindi hiki cha miaka mitano, SMZ imefanikisha kupatikana kwa nafasi za ajira 25,019 Serikalini na katika Sekta Binafsi. Kati ya hizo, nafasi za ajira 4,850 zilikuwa za taasisi mbali mbali za Serikali na nafasi za ajira 20,169 zilitokana na sekta binafsi, zikijumuisha ajira za nje ya nchi na taasisi zinazojitegemea kwa wananchi wa Zanzibar wenye sifa zilizohitajika. Ajira bado ni changamoto Zanzibar na katika nchi za nje hata zile zilizoendelea.

Mafanikio makubwa yanaonekana katika suala zima la masalahi ya wafanyakazi ambapo Serikali imefanikiwa kupandisha mishahara ya watumishi wa umma kutoka kima cha chini cha mshahara wa Tsh.100,000 hadi TZS 125,000 kwa mwezi sawa na asilimia ishirini na tano (25%) pamoja na kufanya marekebisho ya mishahara ya wataalamu na wafanyakazi mbali mbali wakiwemo Madaktari, Walimu wa Sayansi na kadhalika. Serikali ilifanya marekebisho hayo ya mwanzo katika mwaka 2011.

Vile vile, mwishoni mwa mwaka 2013 na mwanzoni mwa mwaka 2014, Serikali ilipandisha kima cha chini cha mshahara kutoka TZS 125,000 hadi TZS 150,000 sawa na asilimia ishirini (20%) pamoja na kurekebisha mishahara ya watumishi wazoefu, waliotumikia katika utumishi wa umma kwa miaka kumi na tano (15) na zaidi ambao wana mishahara kati ya TZS 150,000 hadi TZS 225,000 katika jitihada za kunyanyua kipato cha mfanyakazi, Serikali imeidhinisha posho mbali mbali ambazo tayari zimeanza kutolewa. Malimbikizo ya mishahara ya walimu yatalipwa kutoka bajeti ya mwaka wa fedha wa 2015/2016.

**MHESHIMIWA SPIKA,**

Natoa shukurani kwa mara nyengine kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Nane kwa kuendelea kuweka misingi bora ya utawala bora na demokrasia. Kwa hakika mmeweza kutekeleza vyema wajibu wenu wa kikatiba wa kutunga sheria na kuisimamia

Serikali kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 5A(1) na kufafanuliwa kifungu 5A(2) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984.

Katika kipindi cha miaka mitano, mmefanya majukumu yenu kwa kufanya mikutano yenu katika hali ya salama na utulivu. Licha ya kutofautiana kwa hoja na mitazamo kwa baadhi ya masuala muhimu, mmeweza kupitisha miswada ya sheria 63 na baadae iliwasilishwa kwa Rais kwa ajili ya kutia saini na sasa zimekuwa sheria kamili.

Takwimu zinaonesha kuwa katika kipindi hiki cha miaka mitano, maswali 1558 ya msingi na maswala ya nyongeza (3103) yameulizwa kwa Serikali na yalipatiwa majibu sahihi. Kamati teule 5 mlizoziunda nazo zimetekeleza majukumu yake kwa uadilifu na umakini mkubwa. Nawapongeza wajumbe wote wa kamati teule hizo kwa kufuatilia na kuibua masuala juu mambo mbali na kuyaleta Barazani kwa kujadiliwa na baadae kuishauri Serikali juu ya mambo yanayoibuka. Aidha, nalipongeza Baraza kwa kupokea na kujadili hoja binafsi zinazowasilishwa.

Baraza hili la Nane limeingia katika historia ya nchi yetu, na litakumbukwa kwa kipindi kirefu kijacho katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushiriki katika Bunge Maalum la Katiba kwa lengo la kuunda Katiba Inayopendekezwa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda nikushukuruni nyote Waheshimiwa Wajumbe kwa ushiriki wenu huo uliotuwezesha kupata Katiba Inayopendekezwa ambayo hivi sasa wananchi wanaisubiri kwa hamu kuipigia kura ya maoni.

Leo ni siku ya furaha kwa upande mmoja na siku ya huzuni kwa upande mwengine. Nasema hivi kwasababu tunalivunja Baraza hili kwa mbwembwe na madaha kutokana na mafanikio makubwa tuliyoyapata katika kuiendeleza nchi yetu. Leo ni siku ya huzuni kwa sababu tunaagana na nitalivunja rasmi Baraza hili la Nane na huenda ikapita kipindi bila ya baadhi yetu

kuonana ingawa tunategemeana kwa kiasi kikubwa.

**MHESHIMIWA SPIKA,**

Kwa wale wenye dhamira ya kurejea majimboni kwa ajili ya kutafuta ridhaa ya wananchi kwa mara nyengine, nawatakia mafanikio ili warudi tena kwa miaka mitano myengine.

Kwa wale ambao wamefikia uamuzi ya kutogombea tena, nawasihi waendelee kutumia maarifa na uzoefu walioupata katika baraza hili katika kuongoza, kuhamasisha na kushiriki kikamilifu katika harakati za maendeleo ya nchi yetu. Nyote mtabaki kuwa hazina kubwa katika kupanga na kutekeleza mipango ya nchi hii.

Hata hivyo, kwa wale mtakaojaaliwa kuchaguliwa tena na wananchi na kurudi Barazani, nataka nikunasihini na nikukumbusheni kuwa mnapokuwa kwenye Baraza hili muendelee kuizingatia, kuitii na kuitekeleza kwa vitendo Katiba ya Zanzibar, sheria ziliopo na kanuni za Baraza hili. Baraza la Wawakilishi ni muhimili uliowekwa ndani ya Katiba. Hiki ni chombo kikubwa kinachoendeshwa kwa misingi ya Utawala Bora. Hakiendeshwi kwa kuendesha migomo au njia nyengine yoyote ya ubabe. Baraza ni chombo cha wananchi wa Zanzibar kwa hivyo, suala lolote lenye maslahi ya wananchi, hapa ndipo pahala pa kisheria pakulizungumza jambo hilo.

Kutoka nje ya Baraza si ufumbuzi wa tatizo linalohusu hoja inayojadiliwa Barazani au hoja nyengine iliyokuwa haijadiliwi na Baraza. Waheshimiwa Wajumbe nyinyi ndio mnaotunga sheria za nchi, kwa hivyo nakunasihini msichanganye mambo. Kila sheria iliyotungwa na Baraza hili matumizi yake yako wazi kwa kupitia taasisi iliyowekwa. Nyinyi ni Waheshimiwa na wananchi na jamii kwa jumla wanakuheshimuni na vile vile wanaliheshimu Baraza letu. Ni matarajio yangu kwamba nanyi Waheshimiwa mtairejesha heshima hiyo kwao kwa kuwatimizia matarajio yao ili tupate maendeleo zaidi.

**MHESHIMIWA SPIKA,**

Kila mmoja wetu anaelewa kwamba Baraza lako linaendeshwa kwa misingi ya Sheria na Kanuni. Hoja zinazotolewa na kujadiliwa na baraza hili zinaendeshwa kwa misingi hiyo. Wakati Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa chama cha CUF waliposusia kikao cha tarehe 23 Juni, 2015, hoja walizozitoa hazikuwa na mnasaba na hoja iliyokuwa imewasilishwa barazani ili ijadiliwe kwa wakati huo. Siku hiyo Waziri wa Fedha alikuwa amewasilisha hoja ya kujadiliwa kwa Mswada wa Sheria ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ambao haukuwa na uhusiano wowo hata kidogo na masuala ya kujiandikisha katika daftari la kudumu la kupiga kura. Hoja yao ikuwa inahusiana na Sheria nyengine, Sheria ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Nam. 9 ya mwaka 1992 inayosimamiwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar pamoja na Sheria ya Usajili wa Mzanzibari Mkaazi, Nam. 7 ya mwaka 2005. Waheshimiwa Wajumbe msichanganye mambo.

**MHESHIMIWA SPIKA NA WAHESHIMIWA WAJUMBE,**

Uwamuzi wao wa kutoka nje ya Baraza haukuzingatia uwamuzi wetu wa kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

**MHESHIMIWA SPIKA,**

Uwamuzi wao wa kutoka nje haukuzingatia mapenzi tuliyoyajenga baina yetu.

**MHESHIMIWA SPIKA,**

Uwamuzi wao wa kutoka nje haukuzingatia umoja wetu mshikamano wetu tulioujenga katika miaka mitano.

**MHESHIMWIA SPIKA,**

Uwamuzi wao wa kutoka nje haukuzingantia sifa tulizozipata Zanzibar kutoka katika Jumuiya ya Kimataifa wa kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

**MHESHIMIWA SPIKA,**

Uwamuzi wao wa kutoka nje haukuzingatia maslahi ya Zanzibar.

**MHESIMIWA SPIKA NA WAHESHIMIWA WAJUMBE,**

Tuwaulizeni wenzetu wa CUF ambao tuliamua kwa pamoja kuianzisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa mujibu wa Katiba na Sheria za Zanzibar, tuwaulize, kutoka hapa tulipofika tunakwenda wapi, hatima ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa ikoje sasa, Wananchi wa Zanzibar wana hatima gani ya nchi yao sasa, waulizeni maendeleo tuliyoyapata miaka mitano hatima yake ikoje, tuwaache wananchi waamue na wananchi wataamua tarehe 25 Oktoba mwaka huu, Wataamamua kuhusu hatima yao na maendeleo yao ya Zanzibar, watafanya uchaguzi sahihi, watachagua viongozi wanaoweza kuongoza.

Waheshimiwa Wawakilishi mliobakia humu wa Chama Cha Mapinduzi, nataka nikupongezeni sana sana, mmewawakilisha vizuri sana wananchi wa Zanzibar, mmefanya kazi kubwa sana ya kuipitisha Bajeti, mmeudhihirisha usemi wetu 'zege halilali'. Mswaada wa Sheria wa Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2015/2016 mmeupitisha kwa mafanikio makubwa na mbwembwe kubwa sana, tutawahudumia wananchi wa Zanzibar bila ya matatizo.

**MHESIMIWA SPIKA,**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kuhakikisha kila mwananchi mwenye sifa ya kupiga kura anapewa haki yake hiyo. Nawanasihi sana na nawataka sana Wanasiasa wasipotoshe wananchi juu ya haki hiyo. Nawanasihi viongozi wote wa siasa waiache Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ifanye kazi yake ikiwa huru na isiingiliwe kwa namna yoyote ile. Ni wajibu wetu sote kuheshimu sheria na kushirikiana na Tume ili kuhakikisha tunakuwa na Uchaguzi ulio Huru na Haki. Jambo hilo nitahakikisha linatokea, na sio vyenginevyo.

Kuanzia sasa macho ya ulimwengu yanatuangalia. Tumefanya kazi na Jumuiya ya Kimataifa, Mashirika mbali mbali duniani, nimetembea nchi mbali mbali duniani, kote tunakokwenda na wale wanaokuja Zanzibar wanaipa sifa Zanzibar. Nasema tusonge mbele kwa heshima na nia safi ya kuendeleza mafanikio yetu kama nilivyoyaeleza muda mfupi uliopita.



# SMZ imenyanyua maslahi ya wafanyakazi kwa kiasi kikubwa



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk.Ali Mohamed Shein akizungumza wafanyakazi wa taasisi mbali mbali za Serikali na Binafsi wakati wa sherehe za Kilele cha Siku ya Wafanyakazi Duniani zilizofanyika katika Viwanja vya Kiwanda cha Makonyo Wawi, Chake chake, Mkoa wa Kaskazini Pemba tarehe 01 Mei, 2015*

Mei mosi ya kila mwaka ni siku ambayo wafanyakazi dunianikote huadhimisha siku yao ya Wafanyakazi wakikumbuka tukio la maandamano makubwa yaliyofanywa na wafanyakazi wapatao 200,000, ambao waliitisha mgomo kudai haki zao tarehe kama hiyo mwaka 1886 nchini Marekani.

Hapa Zanzibar sherehe hizo mwaka huu zilifanyika rasmi Kisiwani Pemba katika Kiwanda cha Makonyo Wawi, Pemba ambako Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alialikwa kuwa mgeni rasmi na kuwahutubia mamia ya wafanyakazi waliohudhuria sherehe hizo.

Katika hotuba yake, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alibainisha pamoja na mambo mengine, hatua kadhaa ambazo SMZ imeshazichukua baada ya Mapinduzi ya tarehe 12 Januari 1964, lakini zaidi katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa, ambayo yeye mwenyewe amekuwa akiiongoza.

Hatua hizo zimedhihirisha utekelezaji wa ahadi zake kwa vitendo kama alivyoahidi wakati alipokuwa akiiomba ridhaa ya kuiongoza Zanzibar kwa wananchi. Aidha, hatua hiyo kwa mara nyengine tena inathibitisha mafanikio ya utekelezaji wa Ilani ya CCM 2010 – 2015, na ule msemo maarufu wa kiswahili usemao “Ada ya mja kunena, muungwana ni vitendo”.

Katika hotuba yake Mheshimiwa Rais alibainisha wazi jitihada mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika awamu hii ya saba ambazo imekuwa ikizifanya katika kukabiliana na changamoto zinazowakabili watumishi wa umma, walioko katika sekta binafsi pamoja na kuimarisha uhusiano na Shirikisho la Vyama Huru

vya wafanyakazi nchini. Ili kutekeleza kwa ufanisi suala hili, Rais wa Zanzibar amekuwa na kawaida ya kukutana na viongozi wa Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi (ZATUC) mara kwa mara, jambo ambalo limekuwa likimpa fursa ya kubadilishana nao mawazo juu ya mambo mbali mbali yanayowahusu wafanyakazi.

Hatua hiyo inathibitisha kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inapenda kuwasikiliza wafanyakazi wake na wakati wote inaamini kuwa mazungumzo ni njia sahihi za kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili wafanyakazi. Kutokana na kutambua umuhimu huo, SMZ imeridhia Mkataba Namba 87 wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) unaotilia mkazo umuhimu wa uhuru wa vyama vya wafanyakazi.

Ni ukweli uliowazi kwamba mfumo wa ushirikiano baina ya Serikali na Vyama vya Wafanyakazi, katika kipindi hiki cha baada ya Mapinduzi Matukufu ya tarehe 12 Januari, 1964 ni tofauti na ilivyokuwa kabla ya mwaka 1964. Katika wakati tulionao, wafanyakazi ni sehemu ya Serikali inayoongoza nchi, tofauti na ilivyokuwa wakati ule wa kuitumikia Serikali ya kikoloni.

"Huu ni wakati wa kushauriana na Serikali yenu na kufanya kazi kwa maslahi ya wananchi wote. Aidha, huu ni wakati wa kusikilizana na kushauriana baina ya wafanyakazi na viongozi wenu kwa upande mmoja na viongozi wa Serikali kwa upande mwengine; pale zinapotokea changamoto zinazohitaji kutatuliwa." Alisema Dk. Shein kwenye mkutano huo uliojumuisha wafanyakazi kutoka taasisi za umma na binafsi.

Alisistiza kuwa huu ni wakati ambao viongozi wa vyama vya wafanyakazi wanahitajika kuwa karibu na viongozi wa Serikali yao badala ya kufanya migomo kama ule uliofanywa na wafanyakazi wa bandarini mwaka 1948 au kufanya maandamano ya kudai haki za wafanyakazi ndani ya Serikali ambayo wao wenyewe wafanyakazi pamoja kwa kushirikiana na wakulima ndio walioiweka madarakani.

"Nasaha zangu kwa vyama vya wafanyakazi ni kuitumia vizuri fursa ya majadiliano katika kutatua changamoto zinazojitokeza na kuelewa kuwa Serikali na vyama vya wafanyakazi vina wajibu



*Wafanyakazi wakimsikiliza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk.Ali Mohamed Shein wakati wa sherehe za Kilele cha Siku ya Wafanyakazi Duniani zilizofanyika katika Viwanja vya Kiwanda cha Makonyo Wawi, Wilaya ya Chakechake Mkoa wa Kusini Pemba tarehe 01 Mei, 2015*

mmoja wa kuleta maendeleo nchini". Alisema.

Kama kuna mambo ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaweza kujivunia basi ni mafanikio makubwa ambayo imeendelea kuyapata katika kuinua uchumi wa nchi. Hali hiyo imewezesha kuyaimarisha maslahi ya wafanyakazi zaidi ya mara tatu ndani ya kipindi cha miaka minne kwa namna tofauti, jambo ambalo halikuwahi kufanyika ndani ya Serikali ya kikoloni na hata tokea baada ya Mapinduzi ya tarehe 12 Januari 1964.

Kuanzia mwaka wa fedha 2010/2011 Serikali imekuwa ikichukua hatua ya kuongeza maslahi ya watumishi wa umma hapa nchini. Mwezi Oktoba, 2011, Serikali ilifanya marekebisho ya mishahara kwa watendaji wa Serikali wa ngazi mbali mbali ambapo kima cha chini cha mshahara kilipandishwa kwa asilimia 25.

Marekebisho hayo yalizingatia mambo makuu manne ambayo ni kiwango cha elimu, nyongeza ya mwaka, wafanyakazi waliojiendeleza na nyongeza ya muda mrefu wa utumishi. Kwa mujibu wa marekebisho yaliyofanywa, kiwango cha elimu cha mfanyakazi kilitumika kama kigezo cha mshahara wa mtumishi.

Aidha, marekebisho haya yalirudisha nyongeza za kila mwaka kwa wafanyakazi wa Serikali zilizositishwa kutokana na uwezo mdogo wa fedha katika miaka iliyopita baina ya mwaka 2007 hadi 2011. Sambamba na marekebisho hayo, wafanyakazi walioajiriwa kabla ya mwaka 2007 na ambao walijiendeleza baada ya kuajiriwa, walipatiwa nyongeza moja kwa kila miaka miwili ya utumishi wao kati ya tarehe ya kuhitimu mafunzo yao ya mwaka 2007.

Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Serikali ilifanya tena marekebisho ya mishahara kwa kubadilisha kima cha chini cha mshahara na kubadilisha baadhi ya maposho kwa watumishi wake wa ngazi mbali mbali kuanzia mwezi Oktoba, 2013. Hatua hii imechukuliwa baada kuonekana kwamba baadhi ya makundi ya watumishi wa umma hayakufaidika sana na marekebisho ya mwaka 2011, lakini vile vile ni kutokana na kujitokeza



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk.Ali Mohamed Shein akimkabidhi Bi Mwanahamis Kombo Ali wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais Cheti na Fedha tasilim Shilingi Laki Tano katika sherehe za Kilele cha Siku ya Wafanyakazi Duniani zilizofanyika katika Viwanja vya Kiwanda cha Makonyo Wawi, Wilaya ya Chakechake Mkoa wa Kusini Pemba tarehe 01 Mei, 2015*

haja ya kuangaliwa upya kwa makundi mbali mbali ya wataalamu na wale wafanyakazi wenye uzoefu wa muda mrefu.

Serikali iliamua kufanya marekebisho haya ya mshahara ili kuwanufaisha watumishi wote wa umma kiasi kwamba hakuna mtumishi aliyekuwa hakunufaika na mabadiliko haya. Vile vile, ili kuongeza ufanisi na kuwapa moyo watumishi wenye uzoefu wa kuanzia miaka 15 na kuendelea na ambao kiwango chao cha elimu hakizidi ngazi ya Cheti, Serikali imefanya tena mabadiliko ya mshahara kwa watumishi hao.

Katika mabadiliko haya, Serikali imefanya marekebisho ya vianzio vya mishahara kwa baadhi ya kada za kitaalamu zikiwemo madaktari wa binadamu na wanyama, Wanasheria wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mawakili wa Serikali, Wachumi, Wataalamu wa Sayansi na Kompyuta, Wataalamu wa Teknolojia ya Habari na Wataalamu wenye Shahada ya Uzamili (M.Sc.& M.A) na Shahada ya Uzamivu (Ph.D). Aidha, Serikali imeruhusu posho maalum kwa Wakuu mbali mbali na wanaofanya kazi kwenye mazingira maalum.

Sambamba na mabadiliko hayo, Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma imezielekeza Wizara zote kuipitia Miundo ya Utumishi wa wafanyakazi "Scheme of Service" na kuwapanga Watumishi wote wa Umma katika madaraja yao ya kiutumishi kulingana na taaluma na uzoefu walio nao pamoja na kubainisha majukumu yao. Utekelezaji wa agizo hilo umeshaanza.

Hayo yote yamefanyika kutokana na Serikali kutambua na kuthamini mchango wa wafanyakazi katika kusukuma mbele kasi ya maendeleo, na vile vile kutambua kuwa Wafanyakazi ni rasilimali muhimu inayotegemewa na Taifa lolote katika kuongeza uzalishaji mali na kunyanyua uchumi wa nchi. Hatua hiyo ya Serikali ni miongoni mwa jitihada mbali mbali za kuongeza hamasa ya wafanyakazi wake ili wazidi kufanya kazi kwa bidii na moyo wa kujituma. Hatua hizo siyo tu zina lengo la kuthamini mchango wao katika kuongeza tija na ufanisi wa kazi lakini vile vile iwe ni chachu ya kujituma zaidi katika maeneo yao ya kazi.

Ni dhahiri mafanikio hayo yanatokana na juhudi za wafanyakazi wa sekta ya umma na vile vile sekta binafsi kwa kutimiza wajibu wao wa kufanyakazi kwa bidii na maarifa, kuzingatia sheria za matumizi bora ya fedha za umma na udhibiti wa mapato.

Aidha, mafanikio hayo yanatokana na kazi nzuri ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato inayofanywa na wafanyakazi wa Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRB) na Mamlaka ya Kodi ya Mapato ya Tanzania (TRA) ambao wamekuwa wakifanya kazi inayostahili sifa na pongezi nyingi na inayofaa kuigwa na taasisi nyengine.

Kutokana na jitihada hizo za wafanyakazi na wakulima, uchumi wa Zanzibar umeendelea kukua kwa kiwango cha kuridhisha kila mwaka. Ukusanyaji wa mapato ya ndani umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2010/11 Serikali likusanya Tsh. bilioni 181.4, mwaka 2011/12 Tsh. bilioni 212 na katika mwaka 2012/13 zilikuwa Tsh. bilioni 266.2. Hali pia haikuwa mbaya katika mwaka 2013/14, ingawa kiwango cha matumizi nacho kimeongezeka sana na kutoa changamoto kubwa.

Katika mkutano huo wa maadhimisho ya siku ya wafanyakazi Rais wa Zanzibar aliwasihi watumishi wote kuendelea kuwa na subira na kwamba wale wenye malalamiko kufuatia marekebisho ya mishahara yaliyokwishafanywa, wayapeleke katika sehemu zinazohusika ili yafanyiwe kazi na iwapo itabainika kwamba wana stahili zao ambazo zinakosekana kwa makosa, basi aliagiza, watengenezewe malipo yao kwa haraka.

Aliahidi kuwa Serikali itaendelea kuyaangalia na kuyafanya maslahi ya wafanyakazi wake yawe mazuri kadri hali ya uchumi itakavyoruhusu na itafanya kila jitihada ili lengo hilo liweze kufanikiwa, ingawa alikiri kuwa pamoja na mafanikio makubwa yaliyofikiwa, Zanzibar kama zilivyo nchi nyengine, bado inakabiliwa na changamoto zinazowasibu wafanyakazi wa sekta ya umma, sekta binafsi na vile vile kuendelea kuwepo kwa tatizo la ajira hasa kwa vijana. Hata hivyo alisema "changamoto ni sehemu ya maisha kwa hivyo tusikate tamaa".

# Tamasha la Kimataifa la Muziki na Utamaduni wa Afrika Nchini Ujerumani lilivyoitangaza Zanzibar Ulaya




*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na Mkewe Mama Mwanamwema wakiwa katika picha ya pamoja na Waandaaji wa Tamasha la Kimataifa la 27 la Muziki na Utamaduni wa Afrika mara baada ya kulifungua Tamasha hilo tarehe 05 Juni, 2015 mjini Wurzburg nchini Ujerumani. Wengine katika picha ni Waziri wa Habari,Utamaduni, Utalii na Michezo Said Ali Mbarouk na Katibu Mkuu Kiongozi Dk. Abdulhamid Yahya Mzee*

Ni kipindi cha majira ya joto, unawasili Wurzburg- mji mdogo katika jimbo la Bavaria nchini Ujerumani lakini maarufu ulimwenguni na wenye pirikapirika nyingi katika kipindi cha majira ya joto. Unaelezwa kuwa mji umefurika, hoteli na nyumba za kulala wageni zote zimejaa.

Hivi ndivyo inavyokuwa wakati wa majira hayo. Kwa kuwa Tamasha la Kimataifa la Muziki na Utamaduni wa Afrika ndilo linalopendwa na wananchi wengi wa Ujerumani na wengineo barani Ulaya, mandhari ya mji huu wakati wa Tamasha hili huonekana tofauti na nyakati nyengine zote. Tamasha hili hufanyika kila mwaka katika kipindi hicho na hili ni Tamasha la 27 ambalo inasemakana ndio kubwa na la muda mrefu la muziki na utamaduni wa Afrika katika bara la Ulaya.

Maeneo kadhaa ya mji wa Wurzburg yamepambwa kwa matangazo kuhusu Tamasha hilo lakini mara nakutana na tangazo lenye picha ya mkahawa mmoja ulioko baharini juu ya jabali kubwa. Naambiwa mkahawa huu uko huko Michamvi katika Wilaya ya Kusini, Mkoa wa Kusini, Unguja na kuelezwa kuwa ni mashuhuri miongoni mwa watalii wanaotembelea Zanzibar. Hilo ni moja kati ya matangazo mengi yanayotangaza Zanzibar na Tamasha hilo.

Mwaka huu Tamasha hilo limeipa Zanzibar nafasi maalum na kuchukua dhima ya tamasha hilo ambapo 'theme' yake ilikuwa ni Zanzibar: Kisiwa cha maajabu (Zanzibar: The magic island).

Katika kitabu cha maelezo ya Tamasha hilo, mbali ya picha mbalimbali za Zanzibar katika kitabu hicho, ndani yake kuna kijitabu maalum cha kurasa kumi kuhusu Zanzibar (Zanzibar special) kikiwa kimeandikwa kwa lugha ya kingereza na kijerumani.

Kijitabu hicho kinaeleza historia ya Zanzibar na watu wake huku msisitizo ukiwa kuimarisha taswira halisi ya Zanzibar na watu wake kwa sifa na utajiri wa utamaduni, mila, silka na maisha halisi ya wazanzibari.

Katika Tamasha hilo Zanzibar




*Kikundi cha Taarab cha Skuli ya Muziki ya Nchi za Majahazi (DCMA) kikitumbuiza katika Tamasha la Kimataifa la 27 la Muziki na Utamaduni wa Afrika mjini Wurzburg nchini Ujerumani tarehe 05 Juni,2015 ambapo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alikuwa mgeni rasmi.*

iliwakilishwa na ujumbe kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Kamisheni ya Utalii, Kikundi cha Taarab kutoka skuli ya Muziki wa Nchi za Majahazi kinachoongozwa na msanii Matona,Wajasiriamali na Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC).

Tamasha hilo lililojumuisha maonesho ya muziki na shughuli nyingine mbalimbali za utamaduni lilikuwa na umuhimu wa kipekee kwa Zanzibar kwa jinsi ilivyopewa hadhi na fursa ya kujitangaza nchini Ujerumani na duniani kote.

Ikumbukwe kwamba Tamasha hilo lilitangazwa na mashirika mbalimbali ya habari ya kimataifa zikiwemo televisheni hivyo kuipandisha chati zaidi Zanzibar katika medani ya biashara ya utalii.

Ni jambo la kujivunia kuwa washiriki wengi na waliokuja kuona Tamasha hilo mbali ya kuburudika na muziki wa Taarab kutoka Zanzibar lakini waliweza kupata uzoefu wa moja kwa moja wa mila na utamaduni wa watu wa Zanzibar ikiwemo sanaa ya kutia hina kitu kilichovutia watu wengi waliokuja kwenye maonesho.

Katika kusherehesha Tamasha hilo na kuzidi kuipa nafasi Zanzibar, kulikuwepo pia maonesho ya picha kuhusu Zanzibar kutoka kwa wapigapicha mashuhuri wa Ujerumani bwana Mario Gerth na Joachim Schmeisser yaliyopewa jina la “Zanzibar: Traditions at the Gateway to Africa”.

Mhe Rais wa Zanzibar alipata fursa ya kutembelea maonesho ya bwana Mario Gerth yaliyofanyika katika ukumbi mashuhuri wa Spitale uliopo mtaa wa Zeller ambao ni maarufu kwa maonesho kama hayo. Maonesho hayo yalifanyika kuanzia 29 Mei, 2015 hadi 21 Juni, 2015. Maonesho ya mpigapicha Joachim Schmeisser yalifanyika kuanzia 14 Aprili, 2015 hadi 8 Juni, 2015 katika ukumbi wa maktaba ya jiji.

Kwa hivyo, tunaungana na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutoa shukrani za pekee kwa taasisi ya Afro Project waandaaji wa Tamasha hilo pamoja na mji wa Wurzburg kwa kuipa Zanzibar nafasi ya pekee katika Tamasha la mwaka huu.

Mbali ya shukrani hizo, katika hotuba yake ya ufunguzi Mhe Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alilielezea Tamasha hilo la Muziki wa Afrika nchini Ujerumani kuwa ni tukio muhimu linaloutangaza utajiri na urithi mkubwa wa utamaduni wa bara la Afrika katika ramani ya utamaduni wa dunia.

Kwa hakika, alisema, kuwa ushiriki wa Zanzibar katika Tamasha hilo ni kutekeleza dhamira ya wananchi wa Zanzibar na serikali yao kuimarisha ushirikiano wa kihistoria na urafiki kati yake na Ujerumani na watu wa nchi hiyo. Pia kutoa fursa kwa wananchi wa Shirikisho la Ujerumani ufahamu zaidi Zanzibar na watu wake.

Kwa hivyo alitumia fursa hiyo kuwataka wananchi wa nchi hiyo na nyingine za Ulaya waliohudhuria tamasha na maonesho hayo kuzidi kutembelea Zanzibar kujionea vivutio vingi vya kitalii ikiwemo muziki ambao huoneshwa na kuchezwa katika hoteli nyingi za kitalii Zanzibar.

Akioneshwa kuvutiwa sana na Tamasha hilo, Dk. Shein aliwaambia maelfu ya washiriki na wageni waliohudhuria kuwa ni jambo la

kujivunia sana kuona Tamasha hilo limefanikiwa kuwaunganisha watu wa rangi tofauti lakini wenye dhamira moja ya kuendeleza urithi na ubunifu katika muziki wa Afrika na utamaduni wake.

Aliwaeleza washiriki wa Tamasha hilo kuwa Zanzibar katika historia ya utamaduni wake ilibahatika kutoa wasanii waliotajika ulimwenguni wakiwemo waimbaji Siti binti Saad na Bi Fatma binti Baraka maarufu Bi. Kidude ambaye katika uhai wake alishiriki katika matamasha mengi ya muziki nchini Ujerumani na kwingineko barani Ulaya.

Dk. Shein aliwaeleza washiriki wa Tamasha hilo kuwa kikundi cha Taarab kutoka Skuli ya Muziki ya Nchi za Majahazi Zanzibar kinajumuisha wasanii vijana wenye vipaji ambao wanaendeleza vipaji vyao kwa kujifunza na kuendeleza muziki wa kale wa Zanzibar kama walivyofanya wasanii wa enzi hizo.

Kwa wasanii wa kikundi hicho aliwataka kuitumia vyema fursa waliyopata kudhihirisha umahiri na ustadi wao katika ngazi ya kimataifa katika kutangaza utamaduni wa mzanzibari na pia kujifunza kutoka wasanii wengine walioshiriki tamasha hilo.

Msanii wa kuchora na kupaka hina ambaye pia ni mwalimu katika kituo cha Sanaa na Uchongaji cha Wizara ya Habari,Utamaduni, Utali na Michezo kilichoko Mwanakwerekwe, Bi Mwanakhamis Mohamed Ali anaeleza kuwa maonesho yalitia fora sana na anaamini lengo lililowafikisha Ujerumani limetimizwa.

"Ni mafanikio makubwa kwa upande wangu kuliko sehemu nyingine tulikowahi kufanya maonesho kama haya kwa kuwa watu wa Ujerumani wametuchangamkia sana na walipendezewa sana na uchoraji wa hina" Bi Mwanakhamis aliliambia jarida hili wakati wa maonesho.

Anaeleza watu wengi vijana kwa wazee walifurahia sana sanaa hiyo ya uchoraji hina na aina ya mauwa na kueleza kuwa cha kustaajabisha ni kuwa walikuwa wakitumia muda mwingi kuhakikisha wamepata kile wakitakacho.

"walitumia muda mwingi kupaka, wengine mara tatu ili kukoleza kama tunavyofanya sisi nyumbani na tofauti wanapokuja nyumbani (Zanzibar) watalii wanakuwa hawana muda hivyo wanachora mara moja haraka haraka na kuondoka lakini hapa wanatulia" Bi. Mwanakhamisi anasimulia.

Hata hivyo amependekeza maandalizi zaidi yafanyike katika maonesho kama hayo ambapo kwa upande wa sanaa ya uchoraji hina alipendekeza kuwepo na sehemu maalum yenye stara ili huduma hizo ziweze kutolea kwa kadri ya mahitaji ya wateja.

Wakati tukiwapongeza wasanii wetu walioshiriki Tamasha hilo la 27 kwa kuiwakilisha vyema nchi yetu, kuna haja ya kufikiria kuongeza ushiriki wa Zanzibar kwa kuonesha bidhaa zaidi zenye asili ya Zanzibar ikiwemo mapishi ya vyakula mbalimbali katika maonesho kama hayo. Mbali ya wafanyabiashara kuonesha bidhaa zao lakini pia kuongeza wigo wa mambo ya kuonesha kama vile mapishi ya vyakula mbalimbali vya Zanzibar.




*Mke wa Rais Mama Mwanamwema Shein akimtunza Amina Omar Juma mwimbaji wa Kikundi cha Taarab cha Skuli ya Muziki wa Nchi za Majahazi cha Zanzibar wakati wa ufunguzi wa Tamasha la Kimataifa la 27 la Muziki na Utamaduni wa Afrika tarehe 05 Juni , 2015 mjini Wurzburg nchini Ujerumani ambapo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapindzui Dk. Ali Mohamed Shein alikuwa mgeni rasmi. Kushoto anayetunza pia ni Waziri wa Kilimo na Maliasili Dk. Sira Ubwa Mamboya*

# Ziara ya Rais wa Zanzibar nchini Ujerumani



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na ujumbe wake wakipata maelezo kutoka kwa mmoja wa Maafisa wa Makumbusho ya Viumbe hai ya Berlin Nchini Ujerumani wakati walipotembelea makumbusho hayo hayo nchini humo wakiwa katika ziara ya kikazi, tarehe 09 Juni, 2015*

Hivi karibuni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alifanya ziara ya kikazi katika Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani. Akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kuwasili Zanzibar Dk. Shein aliielezea ziara yake hiyo kuwa ni ya mafanikio makubwa. Jarida lako la Ikulu linaeleza zaidi kuhusu ziara hiyo.

Kumbukumbu za historia zinaonesha kuwa kumekuwepo na uhusiano na ushirikiano wa karibu kati ya watu Zanzibar na Ujerumani kwa karne nyingi tangu enzi ya uchumi wa majahazi wakati huo Zanzibar ikiwa ni kituo kikuu cha biashara katika mwambao wa Afrika Mashariki.

Hata hivyo, kumbukumbu za uhusiano rasmi kati ya Zanzibar na Ujerumani zinaonesha zilianza pale mwaka 1859 wakati mamlaka za miji ya Lubeck, Bremen na Hamburg za Ujerumani zilipotia saini mikataba ya uhusiano wa kibiashara na kidiplomasia na Zanzibar.

Tangu wakati huo uhusiano na ushirikiano huo umepitia katika vipindi tofauti hadi kufikia leo ambapo serikali na wananchi wa Zanzibar na Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani wamekuwa na uhusiano na ushirikiano wa karibu sana.

Kwa hivyo haikuwa jambo la kushangaza pale Rais wa Zanzibar alipoueleza uongozi wa mji wa Wurzburg nchini Ujerumani kuwa "si rahisi kuandika au kuhadithia uhusiano kati ya Zanzibar na Ujerumani na kumtosheleza msikilizaji au msomaji" akimaanisha uhusiano huo sio tu kuwa ni wa karne nyingi lakini umesheheni hazina kubwa ya mambo ambayo watu na nchi hizi wamekuwa wakishirikiana.

Madhumuni ya ziara hii ilikuwa ni kuendeleza na kuimarisha uhusiano na ushirikiano huo lakini mkazo mkubwa

☛ UK.18

# Matukio katika Picha



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza na Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Japan Dk. Batilda Burian aliyeteuliwa hivi karibuni na kufika Ikulu Mjini Zanzibar kujitambulisha, tarehe 6 Mei, 2015



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akisalimiana na mgeni wake Rais wa Msumbiji Mhe. Filipe Nyusi mara baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume kwa ziara ya siku moja hapa Zanzibar, tarehe 18 Mei, 2015



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akimkabidhi zawadi Mwalimu Mkuu wa Skuli ya Bruno H-Burgel ya Postdam Bibi Michael Jungling alipotembelea Skuli hiyo na ujumbe wake katika ziara ya kikazi Mjini Berlin Nchini Ujerumani tarehe 09 Juni, 2015



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza na Balozi wa Malawi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hawa O. Ndilowe alipofika Ikulu Mjini Zanzibar kujitambulisha kwa Rais, tarehe 6 Mei, 2015



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza na Balozi wa Oman Nchini Tanzania Mhe. Saoud Al Ruqaishi alipofika Ikulu Mjini Zanzibar, tarehe 26 Mei, 2015



Mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mama Mwanamwema Shein, akipokea zawadi ya madafu iliyoandaliwa na Vikundi vya Ushirika 32 vilioko Kiwengwa wakati wa kukabidhi misaada kwa vikundi hivyo. Hafla hiyo imefanyika katika viwanja vya mpira Kombaurembo Kiwengwa tarehe 27 June, 2015.




UK.15

*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk.Ali Mohamed Shein akifungua Mkutano wa Wafanyabiashara na Wawekezaji wa Ujerumani wanaowekeza na kufanya biashara Afrika uliofanyika Mjini Berlin, tarehe 10 Juni 2015*

ukiwa katika kukuza ushirikiano wa kibiashara ikiwemo kuhimiza uwekezaji na kuitangaza Zanzibar kuwa kivutio cha biashara ya utalii pamoja na kuendeleza utamaduni.

Kwa hivyo, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na mambo mengine alishiriki matukio makuu mawili muhimu ambayo yalikuwa na mnasaba wa kufikia malengo ya ziara hiyo.

Matukio hayo ni Tamasha kubwa la kimataifa la kila mwaka la Muziki na Utamaduni wa Afrika ambapo Zanzibar ilipewa fursa ya pekee kwa kuwa ndio iliyobeba dhima ya Tamasha hilo na kutoa ujumbe mkuu wa Tamasha 'Zanzibar kisiwa cha maajabu' (Zanzibar: the magic island).

Tukio jingine ni Mkutano wa Wafanyabiashara wa Ujerumani wanaowekeza na kufanyabiashara Afrika. Ni jambo la kujivunia kuwa Mheshimiwa Rais alipewa heshima ya kuwa mgeni rasmi katika matukio yote hayo mawili hivyo ni kudhihirisha sio tu udugu na urafiki wa kweli uliopo kati ya Zanzibar na Ujerumani na lakini pia heshma ya Zanzibar katika medani ya ushirikiano wa kimataifa.

Kwa hivyo matukio haya mawili



*Rais wa wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akimakabidhi zawadi ya mlango wa Zanzibar Dk. Christoph Hauser Naibu Mkurugenzi Mkuu Idara ya Ushikiano wa Kimataifa wa Sayansi baada ya mazungumzo yao walipotembelea Makumbusho katika Mji wa Berlin Nchini Ujerumani katika ziara ya kikazi(kushoto) Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein*

yalikuwa ni fursa adhimu na ya kipekee kwa Zanzibar kwa upande mmoja kuendelea kuimarisha taswira na sifa yake nzuri mbele ya jumuiya ya kimataifa inayotokana utulivu na uzuri wa mandhari yake, ukarimu wa watu wake, mila na desturi adimu za watu wake.

Kwa upande mwingine ilikuwa ni fursa nyingine ya Zanzibar kujitangaza katika harakati zake za kurejesha hadhi yake ya kuwa kituo kikuu cha biashara ambapo kumbukumbu za historia ndio inaifanya Zanzibar hadi leo kufahamika katika ramani ya dunia.

Kwa hivyo, hotuba za Mheshimiwa Rais katika mikutano hiyo miwili zilijielekeza katika kuwashawishi na kuwahamasisha wawekezaji na wafanyabiashara wa Ujerumani na nchi nyingine za Ulaya kuja Zanzibar kwa kuwaeleza kuwa fursa za uwekezaji na biashara zipo na hazina ukomo huku akiwahakikishia mazingira ya uwekezaji kuwa ni mazuri na kubwa zaidi nchi ni shwari na salama.



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na ujumbe waliofuatana katika ziara ya kikazi Mjini Berlin Nchini Ujerumani wakiwa katika picha ya pamoja na Wanafunzi wa Skuli ya Bruno H-Burgel ya Postdam walipotembelea Skuli hiyo yenye ushirikiano na Skuli ya Mwanakwerekwe ya Zanzibar tarehe 09 Juni, 2015*



*Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein akimkabidhi zawadi Naibu Meya wa Mji wa Postdam Bibi Elona Muller alipotembelea Skuli ya Bruno H-Burgel ya Postdam yenye ushirikiano na Skuli ya Mwanakwerekwe Zanzibar akiwa katika ziara ya kikazi Mjini Berlin Nchini Ujerumani tarehe 09 Juni, 2015*

Hotuba yake katika mkutano wa uwekezaji na biashara iligusa washiriki wengi wa mkutano huo matokeo yake Rais wa Chama cha Wafanyabiashara wa nchi hiyo Dk. Stefan Liebing alilazimika kufanya mazungumzo zaidi na Mheshimiwa Rais na kuanisha maeneo ya kipaumbele katika uwekezaji na biashara.

Baada ya mazungumzo ya kina, Dk. Stefan aliahidi yeye binafsi ataongoza ujumbe wa wawekezaji kuja Zanzibar kuendeleza mazungumzo hayo kwa kuangalia fursa zilizopo hasa katika sekta ya nishati, mafuta na gesi pamoja na sekta ya utalii.

Hatua hii inadhihirisha sio tu kazi nzuri iliyofanywa na Mheshimiwa Rais katika kuhimiza uwekezaji na biashara kati ya Zanzibar na Ujerumani bali pia imani waliyonayo wawekezaji na wafanyabishara wa nchi hiyo kwa uongozi wa Dk. Shein.

Itakumbukwa kuwa alipotembelea Zanzibar wakati wa ziara yake katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzaia mwezi Februari mwaka huu, Rais wa Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani Mheshimiwa Joachim Gauck alisifu sana mafanikio ya Serikali uongozi wa Awamu ya Saba inayoongozwa na Dk. Shein.

Rais Gauck alieleza kuwa nchi yake ingependa kuona ushirikiano wake na Zanzibar unaimarishwa na kupanuliwa katika maeneo mengi zaidi kama biashara ya uwekezaji.

Mbali ya kuhimiza biashara na uwekezaji, Dk. Shein alipongeza jitihada za serikali ya Shirikisho la Ujerumani kwa kuendelea kuzisaidia nchi za Afrika katika jitihada zake za kuleta maendeleo ikiwemo kupiga vita maadui watatu ambao ni umasikini, ujinga na maradhi.

Alibainisha kuwa msaada mkubwa wa nchi hiyo kwa nchi za Afrika unaombatana na kusaisda sekta ya elimu, utamaduni, utafiti ni hatua nyingine inayodhihirisha ukaribu wa serikali ya nchi hiyo na bara la Afrika.

Hata hivyo alitoa wito kwa jumuiya ya kimataifa ikiwemo Ujerumani kuwa Afrika ikiwemo Zanzibar inahitaji biashara na uwekezaji si misaada kama



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk.Ali Mohamed Shein na ujumbe aliofuatana nao katika ziara ya kikazi Mjini Berlin wakiwa wamesimama wakisikiliza wimbo maalum na Wanafunzi wa Skuli ya Bruno H-Burgel ya Postdam walipotembelea Skuli hiyo ambayo inaushirikiano na Skuli ya Mwanakwerekwe ya Zanzibar, tarehe 09 Juni, 2015*

ilivyo sasa. Hivyo hivi sasa ushirikiano katika biashara na uwekezaji ni jambo la kipaumbele kuliko wakati mwingine wowote.

"Umefika wakati sasa nchi za magharibi zilenge mbali zaidi kwa kusaidia watafiti wa nchi za Afrika kutengeneza bidhaa zilizoongezwa thamani badala ya nchi hizo kuagiza malighafi kutoka Afrika" Dk. Shein alisisitiza.

Samabamba na wito huo alizisifu nchi za Afrika ikiwemo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mafanikio yao katika kuimarisha uchumi, demokrasia na utawala bora hali ambayo inatosha kuzivutia nchi za magharibi kubadili mtazamo wao kuhusu bara hilo.

"wafanyabiashara wa Ujerumani na wenye viwanda hawana budi kufanya juhudi kuchangamkia mwenendo mzuri wa ukuaji wa uchumi wa Afrika na mazingira ya uwekezaji Zanzibar" Dk.Shein aliuambia mkutano huo wa biashara na uwekezaji.

Mbali ya masuala ya uchumi na biashara, mafanikio mengine ya ziara ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar nchini Ujerumani ni lile la kufanikiwa kuanzisha ushirikiano kati ya Makumbusho ya Historia ya Viumbehai ya Berlin na Zanzibar. Ushirikiano huo unalenga kusaidia kujengea uwezo Zanzibar katika masuala ya uhifadhi, utafiti na mafunzo katika fani ya makumbusho na mambo ya kale.

Kufuatia mazungumzo yaliyofanyika mjini Berlin mara baada ya Mheshimiwa Rais kutembelea makumbusho hayo, ujumbe wa Makumbusho ya Berlin utafika Zanzibar kuja kuangalia mahitaji ya Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale pamoja na kuangalia uwezekano wa kuanzisha mafunzo kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Taifa-SUZA.

Ziara hii inatarajiwa pia kuinufaisha sekta ya afya baada ya mazungumzo ya Mheshimiwa Rais na Ujumbe wa Taasisi ya Afya ya Wurzburg (Mission Medical Institute) ambapo taasisi hiyo ilikubali kuanzisha ushirikiano na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar-SUZA.

Ziara ya Mheshimiwa Rais katika skuli ya Bruno–H-Burgel huko katika mji wa Postdam nayo ilikuwa ya mafanikio Mheshimiwa Rais alisisitiza kuimarisha ushirikiano uliopo kati ya skuli hiyo na skuli ya Mwanakwerekwe ya mjini Unguja ikiwa ni sehemu ya jitihda za wananchi wa Zanzibar na ujerumani kuendeleza udugu na urafiki wao.

Ni ukweli usiofichika kuwa miongoni mwa nchi za Ulaya, Zanzibar inafahamika na kupendwa zaidi nchini Ujerumani. Ingawa kumbukumbu za idadi ya watalii wanaotembelea Zanzibar zinaonesha kuwa Ujerumani ni ya pili baada ya Italia, lakini kutokana na historia ya uhusiano wake na Zanzibar watu wa nchi hiyo wana mapenzi ya dhati na Zanzibar.

Kama alivyowahi kueleza Rais wa nchi hiyo Mheshimiwa Joachim Gauck wakati alipombelea Zanzibar kuwa watu wa Ujerumani wamekuwa wakipata taswira nzuri ya Zanzibar kutokana na watalii wanaotembelea Zanzibar na Tanzania mara kwa mara.

Kutokana na ziara hiyo, matarajio makubwa ni kuimarika kwa ushirikiano kati ya Zanzibar na Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani katika nyanja za uchumi na biashara, uwekezaji, elimu, mila na utamaduni.

Kwa mfano hapana shaka kuwa idadi ya watalii kutoka nchini Ujerumani itaendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka na kusaidia kufikia lengo la serikali ya kuongeza idadi ya watalii 500,000 kwa mwaka wanaotembelea Zanzibar ifikapo mwaka 2015 ambapo hadi mwishoni mwa mwaka 2014 walifikia 311,891.

Kwa upande mwingine matarajio ni kuona ongezeko la kiwango cha uwekezaji kutoka nchi hiyo ambapo hadi sasa kuna miradi 21 yenye thamani ya dola za kimarekani 72 milioni miongoni mwao asilimia 55 ni ya utalii. Hivyo kama ilivyoelezwa awali Zanzibar inatarajia kuona miradi mikubwa ya uwekezaji kutoka Ujerumani katika sekta ya nishati, viwanda na utalii.

Kama alivyoeleza Mheshimiwa Rais mara alipowasili mjini Zanzibar kuwa ziara hii ilikuwa ya mafanikio makubwa na yeye binafsi na ujumbe wake ametiwa moyo sana na taswira nzuri ya Zanzibar iliyojengeka nchini Ujerumani.

Katika mnasaba huo, tunampongeza Mheshimiwa Rais sio tu kwa kufanya ziara hii katika Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani ambayo ni nchi rafiki wa kweli wa Zanzibar lakini vile vile kwa kuweza kufikia malengo ya ziara hivyo kuzidi kuleta matumaini kwa wananchi



# Tuwasaidieni wananchi na hasa wanyonge – Dk. Shein

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Alhaj Dk. Ali Mohamed Shein amewataka wafanyabiashara kuwasaidia wananchi na hasa wanyonge katika mwezi mtukufu wa Ramadhani kwa kuacha kupandisha bei za bidhaa zao kwani alisema, hatua hiyo ni kinyume na malengo ya Serikali.

Akisoma risala ya Mwezi mtukufu wa Ramadhan, Alhaj Dk. Shein amesema Wafanyabiashara wasivutiwe na kutaka kupata faida kubwa katika mwezi huu wa Ramadhani, bali wawafikirie zaidi wananchi wenzao. Ifuatayo ni risala kamili kama ilivyosomwa na

Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Alhaj Dk. Ali Mohamed Shein.

**BISMILLAHI RAHMANI RAHIM**

**Ndugu Wananchi,**

Assalamu Aleikum Warahmatullahi Wabarakatu

Kwa wingi wa heshima na unyenyekevu naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu; Subhana Wataala kwa kutupa rehema na fadhila za kuupokea Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwa mara nyengine tena, tukiwa na amani, utulivu na salama nchini.

**RAMADHAN KARIM.**

Mwenyezi Mungu ametujaaliya mwezi wa Ramadhani kuwa ni mwezi bora kuliko miezi mengine. Huu ni mwezi ambao Yeye Mola wetu ameujaza sifa na sharia Zake kwa aya tano za Surat Al – Baqara, kuanzia Aya ya 183 hadi Aya ya 187. Katika Aya 185 ya Sura hii, Mwenyezi Mungu ameusifu mwezi wa Ramadhani kwa kusema:

"Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa katika mwezi huo hii Kurani ili iwe uongozi kwa watu, na hoja zilizo wazi na uongozi wa upambanuzi (wa baina ya haki na batili)."

Huo ni moja ya Utukufu wa Mwezi wa Ramadhani ambapo Ibada za waja huwa na fadhila kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, tuna wajibu wa kujiandaa na kuweka azma ya kuzidisha Ibada kwa wingi ikiwa ni pamoja na kufanya mambo yote ya kheri, kusali sala za faradhi na sunna na kujifunza na kusoma sana Kurani. Tukumbuke kuwa huu ni mwezi iliyoteremshwa Kurani. Kwa hivyo, kusoma Kurani na kuzingatia mafunzo yake kuna fadhila kubwa. Kadhalika, Aya tulioitaja inatubainishia kuwa Kurani ni uongozi ulio wazi, wa kubaini mambo mabaya tukayaacha na mambo mema tukayaendeleza, ili tuweze kufanikiwa hapa Duniani na kesho Akhera.

**Ndugu Wananchi,**

Ramadhani ni mwezi wa rehema na tunahitajiwa tuzidishe vitendo vya kufanya wema kwa wenzetu, katika biashara na mambo mengine. Aidha, Kurani inatufundisha maadili mema ikiwemo kuwa na moyo wa huruma na kuwasamehe wengine, hasa katika Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani. Pamoja na mambo hayo tunahimizwa kutoa sadaka na kufunga. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa waumini wa kweli na wenye kutekeleza mafundisho ya Kurani kama ilivyoelezwa katika Aya ya 92 ya Surat Al – Imran.

"Hamtaweza kuufikia wema mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda (nguo, vyakula, pesa) na chochote mnachokitoa, basi hakika Mwenyezi Mungu anakijua". Tukumbuke kila tunapotoa, Mola wetu atalipa kheri na hayo yameelezwa sana katika Qurani na Hadithi za Bwana Mtume (S.A.W).

Kadhalika, Mola wetu (SW) ametuambia katika Surat Sab'a, Aya 39 (Juzuu ya 22), yenye tafsiri isemayo:

"Na chochote mtakachotoa basi Yeye Atakilipa; naye ni Mbora wa wanaoruzuku".

Kwa hivyo, huu ni wakati wa kuwafikiria wengine, hasa wale wenye mahitaji katika kutekeleza saumu zao ili nao waone rehema za Ramadhani. Hili si jambo linalowahusu matajiri au wenye vyeo peke yao. Hazrat Abu Zarri amesema:

"Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.A.W) amesema, usifikirie kuwa kila kitendo kidogo kabisa cha wema ni kuwa kidogo".

Kila anayetoa basi ajue malipo yake ni makubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Ni vyema kutoa kwa kuwapa wanaohitaji hasa kwa jamaa, majirani, marafiki na kadhalika.

**Ndugu Wananchi**,

Katika mazingatio ya kufanya wema (ihsani), na kufuata maadili, yanayotukuzwa katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani, tunapaswa tuzingatie umuhimu wa kudumisha na kukuza amani na utulivu. Ibada ya saumu inahitaji kuwepo kwa utulivu wa nafsi ili kuwapa watu wasaa wa kuitekeleza Ibada hii yenye malipo makubwa kwa Mwenyezi Mungu. Katika kuifikia hali hii, sote tuna wajibu wa kusimamia amani na utulivu ili utekelezaji wa ibada zetu usiathirike. Katika kufunga yapo mambo ya kuharibu funga (saumu) ya mfungaji. Miongoni mwa mambo hayo ni kusema uongo na kuwafitini watu. Kwa hivyo, tujiepushe na mambo ya aina hiyo. Lakini, badala yake, tuzidishe mapenzi baina yetu, tuhurumiane na tusaidiane katika mambo yote ya kheri. Tuendeleze utamaduni wetu wa kula pamoja, kufutarishana na kupelekeana vyakula vya tunu. Mambo haya yana umuhimu katika kuendeleza mila na tamaduni njema za Wazanzibari. Tumuombe Mwenyezi Mungu atupe uwezo wa kuyafanya hayo.

Wakati huo huo, nawanasihi wenye kumiliki mikahawa washirikiane na waumini wanaoutukuza Mwezi huu Mtukufu katika kuondoa kero ambazo zinaweza kuwasababishia karaha wanapoitekeleza ibada ya funga. Tudumishe utamaduni wetu wa kuheshimu dini. Jambo ambalo limechangia kudumu kwa amani ya nchi yetu tangu kale na dahari. Kila mmoja anapaswa kuhakikisha kuwa Mwezi wa Ramadhani unaheshimiwa kwa vitendo.

Kadhalika, wazazi nao wanapaswa wawe waangalifu kwa watoto wao nyakati za usiku, ili wawe na nyendo njema pamoja na kuwashajihisha kufanya ibada na kuhudhuria darsa misikitini.

Vile vile, vyombo vyetu vya ulinzi havina budi viimarishe doria za ulinzi katika maeneo yetu mbali mbali, hasa kwa wakati ambao watu wengine wanakuwa katika shughuli za Ibada. Zaidi ya hao, nawakumbusha madereva wazingatie sheria za usalama wa barabarani kwa kutoendesha gari na vyombo vyengine kwa mwendo wa kasi; kwa kisingizio cha kutaka watu wawahi kufutari na kupakia abiria zaidi, jambo ambalo huhatarisha usalama wao. Askari wa usalama barabarani na taasisi nyengine zinazohusika zina wajibu wa kulisimamia suala hili ipasavyo.

**Ndugu Wananchi,**

Kama tunavyofahamu, kwamba mahitaji huwa ni mengi zaidi katika mwezi wa RamadhanI. Kwa baraka za Mwenyezi Mungu, tulijaaliwa kupata mvua ambazo wakulima walizitumia vyema na tumeweza kupata mazao mbali mbali ya chakula yakiwemo yale ambayo huwa yanatumika kwa wingi katika kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Sambamba na hilo, Serikali imeendelea kushirikiana na wafanyabiashara wetu katika utekelezaji wa sera ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kutoa unafuu wa kodi katika uingizaji nchini wa bidhaa muhimu za chakula ikiwemo mchele, unga wa ngano, sukari na tende. Lengo la uamuzi huu wa Serikali ni kuhakikisha kuwa chakula cha kutosha kinakuwepo katika kipindi chote cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na kinapatikana kwa bei nafuu.

**Ndugu Wananchi,**

Kama nilivyoeleza katika miaka iliyopita, napenda nitumie fursa hii tena kwa mwaka huu niwakumbushe wafanyabiashara wote kuwa msipandishe bei za bidhaa zenu bila ya sababu za msingi. Wafanyabiashara wasivutiwe na kutaka kupata faida kubwa, bali wawafikirie zaidi wananchi wenzao. Si jambo la busara kuutumia mwezi huu kwa kuwapandishia bei wananchi, hasa wanyonge. Hatua hiyo ni kinyume na malengo ya Serikali ya kupunguza unafuu wa kodi kwa bidhaa za chakula. Kwa bahati mbaya wapo baadhi ya wakulima wenye tamaa ambao huamua kuleta sokoni mazao ambayo hayajapea. Wakulima hawa si waadilifu kwa hivyo, taasisi zinazohusika zina wajibu wa kusimamia taratibu na utekelezaji wa Sheria ya kumlinda mtumiaji, ikiwa ni pamoja na kuwaepusha kuuziwa bidhaa ambazo muda wake wa matumizi umemalizika.

Ni dhahiri kuwa katika Mwezi wa Ramadhani shughuli za biashara huimarika zaidi. Nawanasihi wafanyabiashara kuendelea kuzingatia sheria. Biashara zote zifanywe katika maeneo yaliyoruhusiwa ili kuepusha usumbufu na msongamano usio wa lazima. Kadhalika, wafanyabiashara pamoja na wafanyakazi wa Baraza la Manispaa kwa mji wa Unguja na Mabaraza ya Miji ya Pemba, waongeze juhudi zao katika kuimarisha usafi wa miji yetu. Uzoefu unaonesha kuwa katika kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani taka huwa zinaongezeka. Kwa hivyo, jitihada zaidi zinahitajika katika kuimarisha usafi wa miji yetu. Tukumbuke kwamba Uislamu unahimiza sana unadhifu.

Kama nilivyoiagiza Mamlaka ya Maji ya Zanzibar (ZAWA) katika Ramadhani za miaka iliyopita na mwaka huu naiagiza tena ZAWA na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kufanya kila jitihada ili iwapatie maji wananchi kwa kutumia magari katika sehemu zote ambazo huduma za maji safi na salama zina upungufu. Natoa wito kwa wananchi washirikiane na Mamlaka hiyo, ili kuifanikisha shughuli hiyo ipasavyo.

**Ndugu Wananchi,**

Wakati tunapokuwa katika Mwezi Mtukufu, ni vyema tukawa tunazingatia matayarisho ya ibada ya Hija kwa wale wanaokusudia kwenda Hija mwaka huu. Muda uliobaki ni mfupi na kutokana na sheria za sasa za Hija, matayarisho yanalazimika kukamilishwa mapema zaidi mwaka huu. Namuomba Mwenyezi Mungu awape baraka wale wote wanaojiandaa na watakaojaaliwa kwenda kuhiji mwaka huu na awajaalie kheri na safari ya salama.

**Ndugu Wananchi**,

Napenda nimalizie risala yangu kwa kukutakieni nyote kheri, rehema na Baraka za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Namuomba Mola wetu atupe nguvu na uwezo wa kuendeleza ibada za saumu, na ibada nyengine katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani pamoja na kudumisha na kuendeleza amani, umoja na mshikamano. Tumuombe Mwenyezi Mungu atujalie Ramadhani njema.

**Ahsanteni**,

**RAMADHAN KARIM**
**Wassalamu Aleikum**
**Warahmatullahi Wabarakatu**

# Mafanikio ya sekta ya afya Zanzibar



*Jengo jipya la kitengo cha maradhi ya Ubongo na Uti wa mgongo liliopo katika hospitali kuu ya Mnazi mmoja, Mjini Unguja*

Uimarishaji wa huduma za afya nchini ni miongoni mwa vipaumbele vya Serikali ya Mapinduzi, Awamu ya Saba na Shabaha ya Mapinduzi ya mwaka 1964. Miongoni mwa jukumu la msingi la Serikali lilikuwa ni kuyaendeleza mafanikio ya Sekta ya Afya ya Awamu zote za Serikali zilizopita na kutekeleza mikakati ya mipango ya Kitaifa kupitia Ilani ya Uchaguzi ya CCM, MKUZA II, Dira ya 2020 na Malengo ya Milenia pamoja na kuhakikisha Sera ya Afya inatekelezwa kwa vitendo kwa kushirikiana na wananchi.

Miongoni mwa malengo makuu ya Serikali yalikuwa ni kuimarisha huduma za Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja ili ifikie kuwa Hospitali ya Rufaa, kuiimarisha Hospitali ya Abdalla Mzee na Hospitali ya Wete ili zifikie hadhi ya kuwa Hospitali za Mkoa. Kwa upande wa Hospitali ya "Cottage" ya Kivunge na Makunduchi kwa Unguja na Micheweni na Vitongoji kwa Pemba, Serikali ilikusudia zifikie hadhi ya Hospitali za Wilaya. Hospitali ya Koteji ya Makunduchi imepiga hatua mbele zaidi. Malengo mengine ni kuanzisha Vitengo vya matatizo ya Figo, Maradhi ya Moyo na Saratani ili huduma hizo ziweze kupatikana nchini pamoja na kuziimarisha huduma za kinga na tiba.

Mabadiliko makubwa yamefanywa katika kipindi cha miaka mitano katika kuimarisha mazingira na huduma zinazotolewa katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja ili ifikie hadhi ya Hospitali ya Rufaa. Hatua zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na kuipatia Hospitali hiyo vifaa vya kisasa katika Chumba cha Upasuaji, Maabara ya Uchunguzi wa maradhi, Wodi ya Wagonjwa Mahatuti, Wodi ya Wazazi na Chumba cha Wagonjwa wa dharura.

Jengo jipya la huduma za upasuaji wa Kichwa na Uti wa Mgongo limefunguliwa likiwa ni la huduma za aina yake katika Afrika ya Mashariki. Kituo cha Meno cha Tabasam kwa ajili ya kuwahudumia watu wenye matatizo ya midomo nacho kimeanzishwa.

Vile vile, Serikali imeanzisha Kitengo cha uchunguzi wa maradhi ya mfumo wa chakula pamoja na Wodi mpya ya Wagonjwa Mahututi. Hivi sasa, Serikali inaendelea na mradi wa ujenzi wa jengo jipya la watoto ambalo pia litakuwa na huduma za wagonjwa wa maradhi ya figo. Ni jambo lilio wazi kuwa huduma katika Hospitali ya Mnazi Mmoja zimeimarika sana na zimepunguza kwa kiasi kikubwa idadi ya wagonjwa ambao walikua wakifuata baadhi ya huduma nje ya Zanzibar.

Serikali inaendelea na ujenzi mkubwa wa Hospitali ya Abdalla Mzee Pemba kwa kuiwekea miundo mbinu ya kisasa na vifaa ili iweze kukidhi kuwa Hospitali ya Rufaa Pemba. Katika Hospitali ya Wete, huduma zimeimarishwa za shughuli za uchunguzi wa maradhi mbali mbali, ujenzi wa jengo la maabara mpya umekamilika. Wodi mpya ya wazazi, wodi ya wagonjwa wa akili na chumba cha upasuaji zimejengwa.

Sambamba na jitihada hizo, jitihada za Serikali katika kuzidisha mwamko wa wananchi juu ya elimu ya afya zimechangia sana kuimarisha huduma hizo na kuongezeka kwa asilimia ya mama waja wazito wanaojifungua katika vituo vya afya hadi kufikia asilimia 68.3 mwaka 2014. Hivi sasa huduma za kujifungua zinapatikana bure katika vituo 41 nchini.

Vifo vya watoto wanaozaliwa hai chini ya umri wa mwaka mmoja vimepungua kutoka 54/1000 mwaka 2010 hadi 46/1000 mwaka 2012 zaidi ya lengo lililokuwepo la vifo 48/1000. Vile vile kuna mafanikio

katika kupunguza vifo kwa watoto chini ya umri wa miaka 5 kutoka 73/1000 mwaka 2010, 66/1000 mwaka 2012. Lengo ni kufikia 50/1000. Vifo vya kinamama kutokana na uzazi vinazidi kupungua.

Kadhalika, Serikali imeendelea kudhibiti kiwango cha Malaria na VVU/UKIMWI kuwa chini ya asilimia moja. Kwa mujibu wa tathmini ya kiwango cha maambukizo ya VVU, Zanzibar inakisiwa kuwa na asilimia 0.5 ya maambukizi kwa watu wenye umri kati ya miaka 15 hadi 24, asilimia 0.6 kwa wenye umri kati ya miaka 15 hadi 49.

Katika kipindi hiki Serikali imejenga ghala la kisasa la kuhifadhia dawa katika eneo la Maruhubi. Serikali za Marekani na Denmark zimesaidia ujenzi huu. Vile vile, Ofisi ya Mkemia Mkuu hivi sasa imehamishiwa katika eneo hilo ili kupata fursa ya kufanya shughuli zake katika mazingira yaliyo bora zaidi.

Jitihada kubwa zimefanywa katika kukiimarisha Chuo cha Taaluma ya Sayansi za afya. Mafanikio yamepatikana ambapo kwa sasa idadi ya madaktari wazalendo imefikia 102. Tunategemea idadi hiyo itaongezeka hasa baada ya Serikali kuamua kuanzisha mafunzo ya udaktari katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na wanafunzi wanaosomea udaktari Tanzania Bara na nje ya nchi.

Kwa wastani daktari mmoja alikuwa akihudumia wagonjwa 31,838 (1:31,838) mwaka 2010 na ambapo sasa anahudumia wastani wa wagonjwa 18,810 (1:18,810). Pamoja na madaktari wazalendo, wapo madaktari wa kigeni 20 kutoka China na 20 kutoka Cuba. Idadi hii inafanya madaktari wote kuwa 151 ambapo wastani wa daktari mmoja anahudumia watu 9,093 (1:9,093).

Akilivunja Baraza la nane la Wawakilishi la Zanzibar, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein ametoa shukrani maalum kwa washirika wa maendeleo wanaoiunga mkono Serikali katika azma yake ya kuziimarisha huduma za afya nchini.


"Tunathamini sana misaada yao ya mafunzo na utaalamu, vifaa, wafanyakazi na nyenzo mbali mbali ambazo kwa pamoja zimeweza kutuletea mafanikio tuliyoyapata." Alisema.

Zanzibar ina mtandao mzuri wa huduma za afya zinazotolewa katika hospitali na vituo vya afya vya Serikali, Vikosi vya Ulinzi, Taasisi za Kijamii na vituo vya watu binafsi kuliko nchi nyingi. Katika Bara la Afrika; mwananchi wa Zanzibar hatembei umbali wa kilomita tano, bila ya kupata huduma za afya kwenye kituo cha afya.

Katika hatua nyengine ya kuimarisha sekta hiyo, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein ametoa pongezi maalum kwa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa kuendelea kuiunga mkono Zanzibar katika kuimarisha sekta ya afya na sekta nyengine za kiuchumi, michezo na utamaduni.

Akizungumza na madaktari wa China waliokwenda Ikulu kumuaga baada ya kufanyakazi Zanzibar kwa kipindi cha miaka miwili, Dk. Shein alisema utamaduni wa kuwaleta Madaktari bingwa kutoka China umeleta mafanikio makubwa katika kutoa huduma za afya hapa Zanzibar.

Amezitaja huduma za upasuaji kwa maradhi ya ubongo na uti wa mgongo kuwa ni huduma zilizoimarika sana na kwamba hivi sasa zinaweza kutolewa hapa Zanzibar kinyume na ilivyokuwa kabla, ambapo wagonjwa walilazimika kufuata huduma hizo nje ya Zanzibar. Hatua hiyo siyo tu imeondoa usumbufu kwa wagonjwa wanaosumbuliwa na maradhi hayo, lakini vile vile imepunguza gharama kubwa ambayo Serikali ililazimika kuingia kwa kuwasafirisha wagonjwa nje ya Zanzibar.



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza na Madakitari wa Kichina kundi la 25 waliopo Zanzibar waliofika kumuaga baada ya kumaliza muda wao wa kazi katika Hospitali mbali mbali Unguja na Pemba. Wa pili kulia ni Balozi mdogo wa China Nchini Tanzania anayefanyia kazi Zanzibar Mhe. Xie Yunliang, tarehe 16 Juni, 2015*



*Mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mama Mwanamwema Shein, akitia saini kitabu cha wageni mara baada ya kuwasili katika viwanja vya Kombaurembo Kiwengwa kukabidhi misaada kwa Wanawake wa Vikundi vya Ushirika 32 vya kijiji hicho. Hafla hiyo imefanyika tarehe 27 June, 2015*

# SACCOS zitumike kuzalisha ajira binafsi

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekuwa ikichukua juhudi mbali mbali katika kuhakikisha kuwa inafanikisha azma yake ya kupunguza na hatimaye kuondosha kabisa tatizo la ajira, ambalo limekuwa likileta changamoto kubwa kwa wananchi wa Zanzibar na hasa vijana na wanawake.

Katika jitihada hizo, Serikali imekuwa ikiwahamasisha wananchi kuanzisha vikundi vya ushirika vya SACCOS, ambavyo tayari vimeonesha mafanikio ya kupigiwa mfano huko Tanzania Bara na baadhi ya nchi nyengine katika Bara la Afrika, licha ya kuweko kwa baadhi ya changamoto zinazotokana na ukosefu wa uaminifu katika utunzaji wa fedha, na elimu ndogo katika suala zima la usimamizi wa miradi.

Akizungumza na wanaushirika wa vikundi mbali mbali vya SACCOS katika hafla ya kuhamasisha vikundi vya ushirika vya Mkoa wa Kaskazini Unguja tarehe 27 Juni, 2015, Mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mama Mwanamwema Shein amewanasihi akinamama kuzitumia fursa zilizopo ambazo Serikali imeziandaa kupitia Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma pamoja na Wizara nyengine ambazo zinahusiana na shughuli zao za maendeleo.

Ili kukuza taaluma katika vikundi vya ushirika na SACCOS zilizopo nchini, Serikali imeandaa mpango mkuu wa mafunzo wa miaka mitatu (Training Master Plan), pamoja na kuandaa miongozo ya aina 13 ya kufundishia kwa mujibu wa mahitaji ya mafunzo yaliyoibuliwa. Mpango huu ni maalum katika kukabiliana na tatizo la ajira Zanzibar ambalo ni moja kati ya vikwazo vya maendeleo.

Hatua nyengine kubwa iliyochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na tatizo hilo katika kipindi cha miaka mitano ni kuanzisha Mfuko wa Uwezeshaji hapo tarehe 21 Disemba, 2013 ukiwa na jumla ya fedha TZS bilioni 2.413, baada ya kuunganishwa Mfuko wa Kujitegemea, Mfuko wa JK na AK na Mfuko wa Vijana.

Kati ya fedha hizo, TZS milioni 973 zilipatikana kwa kuchangishwa kupitia Kamati iliyoundwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, TZS bilioni 1.2 zilitokana na mfuko wa AK/JK na jumla ya TZS milioni 140 ni za Mfuko wa Rais wa Kujitegemea na TZS milioni 100 zilitokana na Mfuko wa Vijana.

Lengo kuu la kuundwa Mfuko wa Kujitegemea ni kuwa na Mfuko ulio imara zaidi katika kuwasaidia vijana, wanawake na vikundi mbali mbali vya wajasiriamali katika shughuli zao za kujiendeleza kiuchumi.

Vile vile katika kuhakikisha kuwa vijana wanapata fursa za ajira, SMZ imefanikiwa kuzindua Mpango Mkakati wa Ajira kwa vijana wa mwaka 2014/2018, ambao umeweka vipaumbele katika sekta za ujasiriamali, elimu ya amali pamoja na ufundi stadi. Mafanikio yameonekana wazi wazi katika kutekeleza Programu ya Ajira



*Mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mama Mwanamwema Shein, akiwahutubia Wanawake wa Vikundi vya Ushirika 32 vilioko Kiwengwa wakati wa kukabidhi misaada kwa vikundi hivyo. Hafla hiyo imefanyika katika viwanja vya mpira Kombaurembo Kiwengwa tarehe 27 June, 2015. Kushoto ni Mke wa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mama Asha Suleiman Iddi*

kwa vijana katika sekta ya kilimo kupitia mashamba darasa, shughuli za uvuvi, ufugaji na utalii.

Aidha, katika kipindi hiki cha miaka mitano Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanikisha kupatikana kwa nafasi za ajira 25,019 Serikalini na katika Sekta Binafsi. Kati ya hizo, nafasi za ajira 4,850 zilikuwa za taasisi mbali mbali za Serikali na nafasi za ajira 20,169 zilitokana na sekta binafsi, zikijumuisha ajira za nje ya nchi na taasisi zinazojitegemea kwa wananchi wa Zanzibar wenye sifa zilizohitajika.

Pamoja na juhudi hizo, tatizo la ajira bado linaonekana kuwa ni kikwazo cha maendeleo na ni dosari katika kukuza pato la taifa. Mpango wa kuanzisha vikundi vya ushirika vya ujasiriamali ambavyo vitahusika na kufanya shughuli mbali mbali za kibiashara na uzalishaji unaweza kuleta mabadiliko makubwa katika kuinua pato la taifa.

Hata hivyo, mafanikio ya utekelezaji wa mpango huo yanahitaji usimamizi mzuri na uhamasishaji wananchi mambo ambayo hayana budi kwenda sambamba na kuonesha mafanikio ya shughuli wanazozifanya baadhi ya watu kwa lengo la kuwatia ari watu ambao wanachukua muda mrefu kufanya maamuzi au wanachelea kukubali kubadilika.

Ni dhahiri kwamba uamuzi wa wananchi walioamua kuanzisha vikundi vya SACCOS hawanabudi kupongezwa kwa uamuaiz wao huo.

Mama Mwanamwema Shein amewapongeza wanavikundi vya ushirika kwa kuamua kuanzisha vikundi hivyo na kusema kuwa uamuzi wao huo unakwenda sambamba na malengo ya Serikali inayoongozwa na Dk. Ali Mohamed Shein wa kuanzisha Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, ambayo inashughulikia masuala ya kuhamasisha na kuendeleza vikundi vya ushirika. Wizara hiyo inatoa huduma mbali mbali, ikiwa ni pamoja na mafunzo, kuvikagua na kuvipatia mikopo nafuu, ili kuwawezesha wananchi kiuchumi.

"Endeleeni kushikamana na viongozi wenu ili mpate maendeleo zaidi. Kumbukeni kuwa "Umoja ni nguvu, na utengano ni udhaifu". Umoja huleta salama na mivutano husababisha hasama". Alisema.



*Baadhi ya Wanawake wa Kombaurembo Kiwengwa walioshiriki katika hafla hiyo tarehe 27 June, 2015*

# Ujenzi holela, uchafu vinachangia maafa yanayotokana na mvua



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akimfariji Bibi Fatma Abdalla Turufino mkaazi wa Uwanja wa Farasi na Kwahani Mjini Zanzibar wakati alipofanya ziara ya ghafla kutembelea wananchi wa sehemu hiyo waliopatwa na maafa ya kuingiliwa na maji ya mvua kubwa iliyonyesha. Ziara hiyo ilifanyika tarehe 05 Mei, 2015*

Mvua ni miongoni mwa neema kubwa za Mwenyezi Mungu alizoziteremsha kwa waja wake duniani. Tumekuwa tukishuhudia maeneo mbali mbali ndani na nje ya nchi ambayo jamii imeathirika hasa kwa ukame kutokana na kukosekana kwa mvua.

Masheikh na maulamaa mara kadhaa wamekuwa wakisalisha sala maalum kuomba mvua zenye kheri pale ambapo kwa bahati mbaya neema hiyo inakosekana kwa muda mrefu na kuashiria ukame unaosababisha njaa na wakati mwengine vifo vya binadamu na wanyama.

Wataalamu wa masuala ya mazingira nao wamekuwa wakichukua juhudi maalum kuishajiisha jamii kuhifadhi mazingira ikiwemo kukata miti ovyo, utiaji moto misitu mambo ambayo yanachangia ukosefu wa mvua na wakati huo huo kuipanda kwa wingi ili kuhakikisha kuwa upatikanaji wa neema hiyo muhimu unakuwa endelevu.

Lakini siyo siku zote mvua hizi zimekuwa zikileta manufaa kwa jamii. Mara kadhaa tumekuwa tukishuhudia maafa yanayotokana na mvua kubwa zinazonyesha. Mafuriko husababisha nyumba kujaa maji na hatimaye kuibua maradhi ya miripuko kama vile matumbo ya kuharisha na kipindupindu, maradhi ambayo husababisha vifo vya binadamu.

Vitabu vitukufu vinatufahamisha kuwa uwezo wa kunyesha mvua unatokana na mwenyewe Mwenyezi Mungu Subhanahu wa Taala. Lakini uzoefu umeonesha kuwa siyo maafa yote yanayotokana na mvua hizo yamepangwa na yeye Muumba. Kwa namna moja au nyengine binaadamu tumekuwa tukichangia sehemu kubwa ya maafa yanayotokana na mvua kwenye maeneo tunayoishi, na ni dhahiri kwamba baadhi ya maafa yanaweza kuepukika iwapo tahadhari za mapema zitachukuliwa.

Ujenzi holela katika maeneo yanayotuama maji au kwenye njia zinazopita maji, kutupa taka ovyo kwenye mitaro inayopitisha maji machafu na maji ya mvua ni miongoni mwa sababu za msingi zinazopelekea kutokea mafuriko kwenye maeneo tunayoishi.

Wakati wa kipindi cha mvua za masika ambazo zimemalizika hivi karibuni tumeshuhudia maafa makubwa yaliyosababishwa na mvua



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akimueleza jambo Mkuu wa Wilaya ya Magharibi Ayoub Mohammed Mahmoud wakati alipotembelea baadhi ya nyumba za wananchi wa Ziwamaboga, Wilaya ya Magharibi zilizoathirika kwa kuingia maji ya mvua na kusababisha hasara mbali mbali. Katika ziara hiyo Mhe. Rais alifuatana na viongozi mbali mbali akiwemo Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Abdalla Mwinyi Khamis, tarehe 05 Mei, 2015*

hizo. Miongoni mwa athari za mvua hizo ni baadhi ya watu kupoteza maisha, maeneo mengi kujaa maji na kuathiri makaazi ya watu, baadhi ya barabara kufurika na kusababisha usumbufu wa usafiri.

Kwa hiyo viongozi wa kitaifa akiwemo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na Mkewe Mama Mwanamwema Shein walilazimika kufanya ziara za kuyatembelea maeneo hayo na kuwafariji walioathirika. Viongozi hao walielezea masikitiko yao makubwa kutokana na maafa yaliyowapata walioathirika na kuahidi kuwa Serikali itahakikisha inawapatia misaada wanayostahiki ili kuwawezesha kurejea katika maisha yao ya kawaida.

Katika ziara hiyo Dk. Shein alitembelea maeneo ya Kwahani, Mwanakwerekwe karibu na Skuli ya Mwanakwerekwe C, Bwawa la Mwanakwerekwe, Tomondo na Kisauni Mtaa wa Ziwa Maboga.

Katika maeneo yote hayo Mheshimiwa Rais wa Zanzibar aliwahakishia wananchi waliopatwa na maafa hayo kuwa Serikali itachukua hatua madhubuti na za haraka ili kuwapatia misaada ya kibinadamu walioathirika ikiwemo chakula na sehemu za kulala kwa wale watakaokuwa hawakubahatika kupata sehemu miongoni mwa ndugu na jamaa zao.

"Tumekuja kuona hali halisi ya maafa yaliyowakuta na Serikali yetu inachukua hatua madhubuti kuwasadia; kwanza kuwapatia makaazi waliokosa kwa jamaa zao na pili kuwapatia msaada wa kukijikimu kipindi hiki cha shida hadi pale mtu atakapojiweza na kurudi katika maisha yake ya kawaida" alisema Dk. Shein. Aidha aliwashukuru wananchi kwa ushirikiano walioutoa kwa wenzao waliopatwa na maafa hayo kwa kuwasaidia sehemu za kuishi kwa muda na hata misaada mingine.

Katika eneo la Kwahani kiasi ya familia 200 ziliathirika huku nyumba 29 wakazi wake wakilazimika kuzihama.

Kimsingi, tatizo la kujaa maji katika mtaa wa Kwahani ni la muda mrefu, lakini limekuwa likiongezeka siku hadi siku kutokana na wananchi kuendelea kujenga bila ya mpangilio na kutupa taka ovyo kwenye mtaro ambao kwa kufanya hivyo, uwezo wake wa kupitisha maji unazidi kupungua.

Eneo la Kwahani halitofautiani sana na baadhi ya maeneo mengine ya mji wa Unguja kama vile Sebleni na Mwanakwerekwe. Tofauti ya maeneo hayo ni kwamba yapo maeneo miongoni mwa hayo siku za nyuma hayakuwa yakipatwa na maafa hayo. Lakini ongezeko la makaazi kutokana na ongezeko la idadi ya watu hasa wale wanaohamia mjini kutoka maeneo mbali mbali na kujenga bila ya mpangilio ndiyo sababu kuu ya maafa kwenye maeneo mapya.

Habari njema kwa wananchi wa Kwahani ni kuwa eneo hilo ni moja kati ya maeneo ya Zanzibar ambayo serikali imepanga kuyageuza kuwa miji ya kisasa yenye kila aina za huduma na kuondokana na kadhia



*Nyumba mbili zinazoonekana kuathirika sana na mvua za Masika za msimu huu katika mtaa wa Mwanakwerekwe baada ya kufanyika shimo kubwa pembezoni mwake pia ni sehemu ambayo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk.Ali Mohamed Shein alitembelea wakati alipofanya ziara ya kuangalia athari za maafa mbali mbali yaliyotokea kutokana na Mvua hiyo, tarehe 05 Mei, 2015*

kama hizo. Mpango huo wa Serikali kwa mara nyengine unawathibitishia wananchi wa Zanzibar dhamira ya dhati ya Serikali kwa wananchi wake. Akizungumza na wananchi wa eneo hilo, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alisema Serikali tayari inao mpango maalum kuhusu eneo hilo ambao utabadilisha kabisa mandhari ya mtaa huo na kuonekana kuwa wa kisasa.

"Ni wajibu wetu kuangalia upya eneo hili la Kwahani na maeneo mengine kama haya ili kuyapatia ufumbuzi wa kudumu kuepuka madhara kama yaliyotokea hivi sasa" alieleza Dk. Shein.

Maafa ya mwaka huu yanayotokana na mvua za masika kwa mara nyengine tena yanatukumbusha umuhimu wa kufuata taratibu za ujenzi kama inavyoshauriwa na Idara ya Ujenzi na Mipango Miji. Ni dhahiri tutaendelea kukabiliana na tatizo hilo kila mvua zitakaponyesha iwapo hatutoachana na tabia ya kujenga kiholela.

Historia inatuonesha kuwa yapo maeneo ya wazi katikati ya mji wa Unguja ambayo kamwe hayakuwahi kujengwa nyumba za makaazi kutokana na unyeti wa maeneo hayo. Kwa bahati mbaya wahamiaji taratibu walianza kuyajenga maeneo hayo. Bahati mbaya zaidi ni kwamba wenye dhamana ya kusimamia ardhi na masuala ya ujenzi wameshindwa kutekeleza wajibu wao na wamekuwa wakiyaangalia maeneo hayo yakivamiwa kama kwamba hawaoni na wengine walihusika katika kuyauza na hata kuyapima na kuyagawa kinyume na sheria.

Wakati umefika sasa kuwachukulia hatua za kisheria wale wanaokiuka sheria na kanuni za Idara ya Mipango Miji lakini vile vile kuwawajibisha wale wanaoshindwa kutekeleza majukumu yao kwani wao ndio wanaopelekea kutokea kwa maafa hayo.

Ili kujiepusha na maafa zaidi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein amezitaka mamlaka husika kuhakikisha kuwa wananchi waliovamia eneo la bwawa la Mwanakwerekwe wanaondoka sehemu hiyo mara moja.

Katika ziara yake hiyo, Dk. Shein alishuhudia eneo la Mwanakwerekwe ambapo ardhi imedidimia kutokana na mvua hizo za masika na kusababisha shimo kubwa ambalo linahatarisha usalama wa nyumba nyingi zilizojengwa katika eneo hilo pamoja na wakazi wake.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Dk. Khalid Salum Mohamed, eneo hilo linahitaji kufanyiwa utafiti wa kina kwa kuwa miaka si mingi iliyopita, jirani na eneo hilo ardhi ilididimia na kutengeneza shimo kubwa kama ilivyotokea sehemu hiyo. Taarifa zinasema kuwa upo uwezekano mkubwa kwamba kuna njia kubwa



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akitoa maelekezo kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais Mhe. Mohamed Aboud Mohamed (kulia) wakati alipofanya ziara ya hafla kutembelea Bwawa la Maji la Mwanakwerekwe Mjini Unguja kuangalia namna lilivyofurika maji kufuatia mvua kubwa iliyonyesha na kupelekea hasara kubwa kwa wananchi. Ziara hiyo ilifanyika tarehe 05 Mei, 2015*

ya maji kwenye eneo hilo chini lakini kwa bahati mbaya watu tayari juu limeshajengwa nyumba za makaazi.

Katika eneo la Tomondo Dk. Shein aliwatembelea wakaazi wawili Bwana Ali Khamis na Bibi Mwanaisha Takrima Mohamed waliopatwa na madhara baada ya sehemu ya nyumba zao kudidimia chini kutokana na mvua zilizonyesha na aliwataka kuwa na subira na kwamba Serikali iko pamoja nao.

Katika maelezo yake kwa Mheshimiwa Rais, Mkuu wa Wilaya ya Magharibi Bwana Ayoub Mohamed Mahmoud alisema jumla ya nyumba 173 zimeathirika lakini nyumba nne zimeharibika vibaya haziwezi kukalika.

Huko Kisauni Mtaa wa Ziwa Maboga ambako sehemu ya ziwa hilo imevamiwa na wananchi kwa kujenga nyumba za kuishi, maji yalijaa na kuingia katika makazi ya watu na hivyo kusababisha wakazi wa nyumba 21 kuzihama nyumba zao.



*Baadhi ya nyumba za wananchi wa Ziwamaboga Wilaya ya Magharibi zilizoathirika kwa kuingiliwa na maji ya mvua kubwa iliyonyesha kepelekea hasara mbali mbali kwa Wananchi wanaoishi maeneo ya pembezoni mwa ziwa hilo ambapo leo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alitembelea tarehe 05 Mei, 2015*

